# Nipashe

Jumatatu Mei 18, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580234

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710




## Ndugulile afunguka baada ya kutumbuliwa na Rais

UK. 3




UKURASA 11

# JPM asimulia mwanawe alivyougua, kupona corona



**ASEMA** alijifukiza, aanika hali ilivyo nchini, afikiria kufungua vyuo wiki hii, aangiza sukari kutoka Uganda... *Endelea UK. 2*



Mwenyekiti wa Umoja wa Mabenki (TBA) na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Ndekela, akizungumza juu ya mpango wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) katika kuimarisha uchumi katika kipindi hiki ambacho taifa linakumbana na changamoto ya ugonjwa wa corona na namna gani benki zimejipanga katika kufanikisha maazimio ya BoT. Kulia ni Makaumu Mwenyekiti TBA, Sanjay Rhugani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

## BAA LA CORONA



Usifanye mazoezi kama una homa, kikohozi au matatizo ya kupumua. Kaa nyumbani upumzike. WHO

- Epuka mikusanyiko ya watu
- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo

## WAANDISHI WA KENYA MATATANI 'KUPENYA' TANZANIA

UKURASA 4

# Mbowe awataja Mwinyi, Mkapa, Kikwete vita corona

UK. 4




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play · App Store


**MICHEZO** RAIS MAGUFULI ATOA TAMKO LIGI KUREJEA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Vijana wanaofanya kazi ya kupiga debe stendi ya Mafinga wilayani Mufindi, mkoani Iringa, wakifanya majaribio ya kuwapima joto wasafiri katika stendi hiyo, mara baada ya kifaa hicho cha kupimia joto na vifaa kinga vingine vya corona kutolewa na kampuni ya nguzo za umeme ya Qwihaya General Enterprises Ltd juzi. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# JPM asimulia mwanawe alivyougua, kupona corona

**Na Salome Kitomari**

RAIS John Magufuli, jana alisimulia namna mwanawe alivyougua ugonjwa wa corona na kupona kwa kunywa malimao, tangawizi na kujifukiza.

Akitoa salamu zake wakati wa ibada ya Jumapili katika Usharika wa Chato mkoani Geita, iliyoongozwa na Mchungaji Thomas Kangeizi, Rais Magufuli alisema kwamba, mara baada ya mwanawe kugundulika kuwa na virusi vya corona, alijitenga na kuanza kutumia vitu hivyo hadi alipopona na sasa anachapa kazi.

"Mtoto wangu alipata corona, alijifungia amejitibu, kajifukiza, kanywa malimao na tangawizi amepona, yupo mzima sasa anapiga 'push-up', ndiyo ukweli. Siwezi kusema uongo mbele ya madhabahu hii niliyosimama.

"Wapo wanadhani mimi corona haujanipata nyumbani kwangu, niwaambie mtoto wangu wa kuzaa ameugua na amepona," Rais Magufuli alisema.

**WAGONJWA KUNYANYAPALIWA**

Kiongozi huyo wa nchi pia alisimulia namna rafiki yake ambaye ni injinia alivyozungushwa hospitali tofauti jijini Dar es Salaam huku akiambiwa ana corona, lakini baadaye ikagundulika hana maambukizo ya virusi hivyo.

"Yupo rafiki yangu injinia, alipata kiharusi akalazwa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), lakini baada ya siku mbili alipimwa corona wakasema anayo. Akatolewa, akapelekwa Amana (ambacho ni) kituo cha wagonjwa wa corona, akalazwa kwenye kitanda, watu wanamwogopa kwamba ana corona.

"Ndugu zake wakamchukua wakampeleka Aghakhan, akatafutiwa chumba, akaambiwa atoe Sh. milioni sita, familia ikajichanga ikatoa, wakachukua vipimo tena vya corona na hakuwa nayo, wakampeleka wodi ya kawaida na sasa yuko nyumbani amepona, anazungumza," alisema.

Kwa mujibu wa Rais Magufuli, kuna watu wamepoteza maisha kwa kufikiria corona, na kutolea mfano kisa cha wauguzi na madaktari 60 wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) ambao walitakiwa kujitenga kwa kuwa walikutana na wagonjwa wa corona.

MAZISHI YAWE KAWAIDA

Rais Magufuli pia alisema kuwa wapo wanaofariki dunia kwa magonjwa mengine, lakini hospitali zinang'ang'ania kuwapima corona, akihoji sababu za kuchukua vipimo vya mwili wa mtu ambaye ameshakufa.

"Nguvu za kupima anazo ila kumhudumia kabla hajafa hawana, na akipimwa kila kitu kinaandikwa corona na wanazuia ndugu zake kumzika, ni mbinu za ajabu na za ovyo kabisa," alisema.

"Nitoe wito kwa madaktari na Wizara ya Afya, mtu akifariki (dunia), hata kama ni corona, lazima azikwe kwa heshima zote kama kawaida maana corona siyo Ebola, watu wazikwe kwa maziko ya kawaida. Mbona waliokufa kwa surua, TB na Ukimwi hatufanyi hivyo? Haya ni mambo ya ovyo ovyo," alisema.

**'SITAFUNGIA WATU NYUMBANI'**

Rais Magufuli pia alisisitiza msimamo wake wa kutofungia watu nyumbani kwa kuwa ingekuwa utumwa wa hali ya juu, akisema ugonjwa wa corona hauna tofauti na vita nyingine zozote.

"Fikiria ufungiwe usionane na mume au watoto, tumezoea tunakwenda kutafuta chakula kwenda kazini, kuvua, vyote vingezuliwa, tungekuwa tuko wapi Watanzania milioni 60? Huruhusiwi kwenda sokoni halafu usiku hurusiwi kutoka kana kwamba corona inatembea usiku tu," alisema.

Rais Magufuli alisema serikali inatekeleza miradi mingi ya maendeleo ambayo kama nchi ingefungwa, watu walioajiriwa kwenye miradi ya ujenzi wa barabara, kituo cha kufua umeme na reli wasingekuwa na kazi, akitaka kila Mtanzania afikirie hali ingekuwaje.

**MADEREVA KUZUIWA MIPAKANI**

Rais alieleza kushangazwa na madereva kuzuiliwa kuvuka mipaka ya baadhi ya nchi jirani ilhali wameshatembea umbali wa kilomita zaidi ya 1,000 bila kuanguka au kupata madhara yoyote ya kiafya.

"Sijafunga mipaka, niliheshimu wenzangu, ukifunga umeharibu uchumi wao, wanategemea chakula Tanzania kama mahindi, mchele, nyama, maziwa, ukifanya hivyo, utawaumiza," alifafanua.

**HATUJAJITENGA EAC, SADC**

Rais Magufuli pia alitoa ufafanuzi kuhusu madai ya wakosoaji wa serikali yake kwamba imejitenga katika baadhi ya jumuiya za kikanda akisema:

"Hakuna kufunga nchi wala nini na Mungu atatusaidia, wakishamaliza watakuja kuomba chakula na tusiwabague, ndani ya Afrika Mashariki (EAC) tuko pamoja na nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), tupo tunashikamana ila katika kutatua tatizo kila mtu ana njia zake.

**SUKARI YA UGANDA**

Alizungumzia uhaba wa sukari uliojitokeza hivi karibuni nchini, akibainisha hatua zilizochukuliwa kuwa ni pamoja na kuagiza sukari kutoka taifa jirani la Uganda.

"Nilizungumza na Rais wa Uganda, tulikuwa na upungufu wa zaidi ya tani 42,000, ila Uganda uzalishaji ukawa mzuri, nilizungumza na Rais Yoweri Museven, ametuuzia tani 26,000 na sasa hakuna upungufu, ila wanaoficha ni wanafiki, watu wabaya.Je, tungefunga mipaka, tungepata hii sukari?" Alihoji.

## ... afikiria kufungua vyuo wiki hii

**Na Salome Kitomari**

RAIS John Magufuli amesema anafikiria kufungua vyuo nchini wiki hii, iwapo hali ya maambukizo ya virusi vya corona itaendelea kupungua kama ilivyo sasa.

Machi 17, mwaka huu, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alitangaza kufunga shule zote na kusitisha michezo ya aina yoyote nchini na baadaye alifunga vyuo vyote nchini.

Akitoa salamu zake katika ibada ya Jumapili katika Usharika wa Chato mkoani Geita, iliyoongozwa na Mchungaji Thomas Kangeizi, Rais aliwashukuru Watazania na viongozi wa dini kwa kuitikia vyema kufunga na kuomba kitaifa kwa siku tatu ili Mungu ainusuru nchi dhidi ya janga la corona.

Alisema kutokana na mambo makubwa yaliyofanywa na Mungu, sasa ni wakati wa kumshukuru na kwamba ni vyema viongozi wa dini na Watanzania wakaungana katika maombi ya kitaifa ya siku tatu kuanzia Mei 22 hadi 24 ambayo ni mahususi kwa shukrani kwa Mungu.

Rais alitoa takwimu ambazo zilionyesha hadi jana, nchi ilikuwa na jumla ya wagonjwa 144 wa corona katika vituo 14 nchini, na kwamba wengi wao wana hali nzuri na walio na hali mbaya ni kwa kuwa wana magonjwa mengine.

Alijata vituo hivyo kuwa ni Amana ambacho awali kilikuwa na wagonjwa 198, lakini kwa sasa wamebakia 12, Mloganzira iliyokuwa na wagonjwa 30 na sasa wamebakia sita, Kituo cha Lulanzi (Kibaha) walikuwa 50 na sasa wamebakia 22.

Kwa mujibu wa Rais Magufuli, vituo vingine jijini Dar es Salaam na idadi ya wagonjwa kwenye mabano ni Agha Khan (31), Hindu Mandal (16), Regency (17), TMJ (7), Rabinisia (14).

Alisema mkoani Arusha kuna vituo vitatu na idadi ya wagonjwa kwenye mabano ni Moshono (11), Longido na Karatu havina, huku jijini Mwanza kukiwa na vituo 10 na kati yake, Hospitali ya Rufani Bugando na Sekou Toure kuna wagonjwa wawili ambao wanahitaji uangalizi wa karibu kwa kuwa wana magonjwa mengine.

Alisema wagonjwa wengine katika halmashauri nane na idadi yake kwenye mabano ni Buswelu (2), Misungwi (2), huku Ukerewe, Magu, Mkuyuni, Nyahunge, Bochoshe, Sengerema na Kwimba wakiwa hawana mgonjwa hata mmoja.

Jijini Dodoma kuna vituo viwili vyenye wagonjwa wawili ambao wanahitaji uangalizi wa karibu kwa kuwa walikuwa na magonjwa mengine kabla ya corona, na kwamba awali kulikuwa na zaidi ya wagonjwa 40.

Alisema kuwa wilayani Kongwa, Kondoa (Kituo cha Beloko) pia hakuna mgonjwa hata mmoja.

"Mungu amejibu maombi yetu, Mungu ashukuriwe sana kwa kutusikiliza, kwa mwendo huu ninawasisitiza Watanzania kuendelea kuchukua tahadhari na kumwomba Mungu.

"Kwa hali hii ninavyoona kama ikiendelea hivi kwa wiki hii, nimepanga kufungua vyuo ili wanafunzi waendelee kusoma, lakini pia nimepanga kuruhusu michezo iendelee maana ni moja ya burudani kwa Watanzania," alisema.

**WATALII KUANZA KUFURIKA**

Kwa mujibu wa Rais Magufuli, kuna mashirika ya ndege ambayo orodha ya wasafiri imejaa hadi Agosti mwaka huu kwa watalii wengi kukata tiketi kwa ajili ya kuja nchini kwa sababu wameshajua ukweli.

"Nimeshatoa maagizo kwa Waziri wa Maliasili na Utalii kuwa wakija, waruhusie kuingia, hakuna kuwaweka kwenye uangalizi kwa siku 14, mtalii akishapimwa joto aruhusiwe akatalii kwenye hifadhi zetu," alisisitiza.

## Serikali yawatangazia neema wastaafu

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

SERIKALI imewatangazia neema wastaafu, kwa kueleza kuwa mwaka ujao wa fedha imewaweka katika kipaumbele cha kuhakikisha wanapewa mafao yao kwa wakati.

Hivyo, imeendelea kufanya uhakiki wa daftari la pensheni kila mwezi kabla ya malipo, kuandaa vitambulisho vipya vya wastaafu vya kielektroniki katika mfumo wa "smart cards" na kuboresha mfumo unaotumika kutoa huduma kwa njia ya mtandao.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki bungeni wakati akijibu hoja za wabunge waliotaka kufahamu mikakati ya serikali katika kuhakikisha mafao ya wastaafu yanalipwa kwa wakati.

Dk. Mpango alisema kinachochelewesha wastaafu kulipwa kwa wakati ni udhaifu katika taarifa, lakini mikakati inaandaliwa ya kuhakikisha wazee waliolitumikia taifa wanastaafu vizuri na kwa amani.

Waziri Mpango alisema: "Tutajitahidi kadri inavyowezekana wazee waliolitumikia Taifa kwa kweli wanastahili mafao yao wapewe kwa wakati, Kinachotusumbua mara nyingi ni udhaifu katika taarifa, lakini pale wizarani ni moja ya maeneo ambayo tumeyawekea kipaumbele kuhakikisha wastaafu wetu wanastaafu vizuri na kwa amani."

Dk. Mpango alisema wizara inawajibika kulipa mafao na pensheni kwa watumishi wa umma ambao hawachangii katika mifuko ya hifadhi ya jamii, mirathi na malipo ya kiinua mgongo kwa watumishi wa Serikali walio katika mikataba na viongozi wa kisiasa.

Alisema kati ya Julai 2019 na Machi 2020, Wizara imelipa mafao na pensheni kwa wastaafu wa serikali 57,605, mirathi kwa warithi 1,006 na malipo ya kiinua mgongo kwa watumishi 457 wa serikali walio kwenye mikataba pamoja na kuendelea na uhakiki wa daftari la pensheni.

Alisema wizara itaendelea kutoa huduma za pensheni, mirathi, utunzaji wa kumbukumbu na uhakiki wa wastaafu kwa njia ya mtandao na kuwapatia wastaafu vitambulisho vya kielektroniki.

Wakichangia makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/21, wabunge waliitaka serikali kuhakikisha inawajali wastaafu.

Mbunge wa Singida Mashariki (CCM), Miraji Mtaturu, aliiomba Wizara ya Fedha na Mipango kushughulikia kwa haraka mafao ya wastaafu, kwani wastaafu wamekuwa wakitumia muda mwingi kufuatilia.

"Kuna baadhi ya wastaafu wamekuwa wakicheleweshewa kupatiwa mafao yao pindi wanapostaafu, wengi wao wanashindwa kulipwa kwa wakati na wamelitumikia Taifa hili kwa uadilifu mkubwa, niwaombe Wizara ya Fedha tuwe tunawalipa kwa wakati wastaafu," alisema na kuongeza:

# Ndugulile afunguka kutumbuliwa na JPM

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU moja baada ya Rais John Magufuli kutengua uteuzi wa Dk. Faustine Ndugulile katika baraza lake la mawaziri, Mbunge huyo wa Kigamboni, amezungumzia uamuzi huo.

Juzi usiku, Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu, ilitangaza uamuzi huo, ikisema Rais amemteua Mbunge wa Siha, Dk. Godwin Mollel, kuwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Taarifa hiyo ya Ikulu ilieleza kuwa Dk. Mollel anachukua nafasi ya Dk. Ndugulile ambaye uteuzi wake umetenguliwa. Hata hivyo, haikuelezwa katika taarifa hiyo sababu za kutumbuliwa kwa Dk. Ndugulile.

Katika ukurasa wake wa Twitter jana, Dk. Ndugulile alizungumzia kwa kifupi kutumbuliwa kwake, akimshukuru Rais Magufuli kwa kumpa nafasi kutoa huduma kwenye serikali yake.

"Nimepokea uamuzi wa Mheshimiwa Rais kwa unyenyekevu mkubwa. Ninamshukuru JPM (John Pombe Magufuli) kwa kunipa fursa ya kuhudumu katika serikali yake.

"Ninawashukuru sana Ummy Mwalimu (Waziri wa Afya) na watendaji wote kwa ushirikiano walionipatia. Mafanikio ya sekta ni makubwa sana. Ninamtakia kila kheri NW (Naibu Waziri) ajaye; Dk. Mollel," alisema.

Dk. Mollel (40), kabla ya kujiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM) Desemba 2017, alikuwa mwanachama na Mbunge wa Siha mkoani Kilimanjaro kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Kabla ya kukikimbia chama hicho kikuu cha upinzani nchini, Dk. Mollel ambaye kitaaluma ni daktari wa binadamu, alikuwa Waziri Kivuli wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ambako sasa amerejeshwa tena, safari hii akiwa Naibu Waziri.



Mkulima wa mpunga katika skimu ya Kijiji cha Bahi Makulu akikusanya kwenye trubai sehemu ya mpunga kutoka kwenye maji yaliyofunika mashamba ya mpunga zaidi ya heka 11,000 wilayani Bahi mkoani Dodoma. **PICHA PAUL MABEJA**

# KKKT yatoa waraka ikionya matumizi mitandao kijamii

**Na Hamida Kamchalla,**

**TANGA**

KANISA la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini Mashariki, limetoa waraka likionya watu wanaomkashifu askofu wa dayosisi hiyo na uongozi wake kwa kusambaza nyaraka kupitia mitandao ya kijamii.

Hatua hiyo imefikiwa wakati dayosisi hiyo ikielekea kwenye mkutano mkuu wa tatu baada ya miaka 125 ya injili, kukiibuka kundi la watu waliojiita wanadayosisi, wakisambaza nyaraka za kumtaka askofu ajiuzulu.

Akisoma waraka huo mwishoni mwa wiki jijini hapa, Katibu wa Dayosisi hiyo, James Mwinuka, alisema watu hao wamekuwa wakimtukana askofu, wasaidizi wake na halmashauri kuu na kuushinikiza uongozi huo kujiuzulu bila kuweka bayana sababu za msingi zinazowabana viongozi hao kikatiba.

Mwinuka alisema kuwa watu hao walijitambulisha kuwa wanatoka ndani ya dayosisi hiyo, lakini kilichopo dayosisi inaamini hawana nia njema na dayosisi yao kwa kuwa zipo sehemu husika za kuwasilisha malalamiko.

"Tunatambua kwamba wengi wameguswa na kuumizwa na jambo hilo, tunapenda kuwapa pole na kuwatia moyo kwamba Kristo yu pamoja na kanisa lake na kwa moyo wa upendo, kanisa tunawaonya mtu au kikundi hicho cha watu wanaosambaza nyaraka hizo, waache mara moja," alisema.

Askofu wa kanisa hilo, Dk. Stephen Munga, alisema vikwazo kwenye uongozi ni kawaida na hao wanaomlazimisha kujiuzulu wasiwe na uharaka huo kwa kuwa kustaafu kwake ni lazima na anasubiri uchaguzi mkuu wa kumpata askofu badala yake.

Alisema atastaafu kwa utaratibu huo, lakini si kama wanavyotaka hao wanaosambaza nyaraka za vitisho na matusi.

Askofu Munga alisema kwamba anachohitaji ni amani na wakati wa mkutano ukifika, watafanya uchaguzi kumpata askofu mpya atakayekalia kiti hicho na kuongoza vyema dayosisi hiyo.

Aliongeza kwamba, kupewa vitisho na kutukanwa, kumeshawahi kutokea huko nyuma na kusema kuwa ukiwa kiongozi, bila kukubali misukosuko, hauwezi kuhimili uongozi.

"Nina uzoefu mkubwa katika uongozi wangu, nina miaka 30 uchungaji na miaka 20 kwenye uaskofu, sikuwahi kuchoka kwenye uongozi.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2
Katika mahakama ya mwanzo

MJINI-MOROGORO
Usimamizi wa mirathi **No;72/2020**

Ombi la **MUHINA HUSSEIN JUMA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **HUSSEIN JUMA MZIMBA** .

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 18/05/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 15/05/2020.

Sahihi ya Hakimu

**TANGAZO LA KUPOTEA KWA KADI YA GARI.**

ERASTO ZACHARIA MASSANJA
ANATANGAZA
KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NO YA USAJILI T310 BLE
CHASSIS NO SF5-079929,
ENGGINE NO EJ20-551440
SUBARU FORESTE

ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI
DAR/CEN/RB/260072/2019

157433

**MNAYA AUCTION MART COMPANY LIMITED**
P.O. BOX 80896, DAR ES SALAAM
Physical Address: Kibaha Tumbi EX, NBC House 1st Floor.

**Mnada Mnada Mnada**

Kampuni ya Mnaya Auction Mart kwa idhini tuliyopewa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kibaha, itafanya mnada wa hadhara siku ya Alhamisi tarehe 21/05/2020, saa tano asubuhi. Tutauza nyumba iliyopo eneo la Kibaha-Visiga - Zegereni.

Masharti ya Mnada

1. Mnunuzi atatàkiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa
2. Màlipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote, kushindwa kufanya hivyo, mnunuzi atakua amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada kurudiwa.

**Kwa maelezo zaidi piga simu namba 0718 925 291 au 0713 932 566.**

*Wote mnakaribishwa.*

# Chadema yawataja Mwinyi, Mkapa, Kikwete vita corona

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

CHAMA cha Demokrasia na Maendelea (Chadema), kimetoa mapendekezo kadhaa kwa serikali kuhusu namna ya kupambana na ugonjwa wa virusi vya corona, mojawapo ni kuwashirikisha marais wastaafu.

Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Watanzania kupitia mitandao ya kijamii na kueleza kuwa ili kuushinda ugonjwa wa virusi vya corona, kunahitajika ushirikiano wa watu wote.

Katika hotuba yake, Mbowe aliitaka serikali kutokuona aibu katika kuwashirikisha wadau wengine katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo na kwamba isilihodhi jambo hilo bali inahitajika nguvu ya pamoja.

Pia, aliitaka serikali kuzishirikisha taasisi za umma, wasomi wenye mawazo mapana katika kutatua tatizo la uwapo wa ugonjwa wa virusi vya corona.

"Tunapaswa kuwashirikisha marais wetu wastaafu, watupe mtazamo wao, sijamsikia Rais mstaafu Kikwete, Mkapa, Mwinyi wakizungumza kuhusu janga hili, tunapaswa kushirikisha ili tupate mwanga wa wapi pa kuanzia," alisema Mbowe.

Mbowe alisema serikali inapaswa kuwa na utengano wa ushirikiano wa kimataifa katika kupambana na ugonjwa wa corona.

**KUTUNGWA SHERIA**

"Serikali itunge sheria ya Bunge itakayosimamia utekelezaji bora wa vita dhidi ya corona. Sheria hiyo itatoa mwongozo wa kitaifa, siyo sasa hivi kila mtu anazungumza tu, tunapaswa kurejesha ushirikiano na mataifa ya kigeni kuliko kuwaita maadui," alisema Mbowe na kuongeza:

"Tusiwaite mabeberu, tusiwabeze, hao tunaowaita mabeberu, wanabalozi zao hapa nchini, ndiyo hao hao tunaowakilimbilia kuomba misaada."

**KUTENGWA FEDHA**

Aidha, Mbowe alisema serikali inapaswa kutenga rasilimali fedha na wataalamu ambao watashirikishwa katika vita hii.

"Sisemi mimi nahitaji kazi, sihitaji kuwa katika timu hiyo ya wataalamu, lakini ninaamini hapa nchini kuna wataalamu, ndani ya CCM, taasisi za umma kuna watu wenye ujuzi, viongozi wastaafu, magavana wa fedha, wanaweza kushirikishwa katika kutatua changamoto hii," alisema Mbowe.

**KUSHAURIANA NA TAASISI**

Alisema serikali pia inapaswa kuweka mkakati makini wa kushauriana na mashirika ya fedha duniani kama vile, Shirika la Fedha Duniani (IMF), Shirika la Afya Duniani (WHO).

Alisema kuibagua na kutosikiliza ushauri unaotolewa na WHO siyo vizuri kwani kwa kufanya hivyo ni sawa na kuipinga Umoja wa Mataifa (UN) ambayo Tanzania ni mwanachama.

Alisema Serikali inapaswa kuweka mkakati wa makusudi wa kuwalinda wanaopigana na ugonjwa huu wakiwamo madaktari wote wa serikali na umma.

**MAWASILIANO NA NCHI RAFIKI**

Alisema pia serikali ifanye mawasiliano na nchi marafiki ikiwamo Cuba kwa kuomba msaada, kwa sababu urafikiwa Cuba na Tanzania ulikuwapo tangu enzi.

"Pia tunashauri kuwapo na mpango salama wa mazishi kwa wenzetu waliopoteza maisha, pamoja na utoaji wa taarifa za mara kwa mara kuhusu ugonjwa huu," alisema Mbowe.

**UTOAJI ELIMU**

Mbowe alisema serikali inapaswa kuhakikisha elimu na kampeni ya kupambana na ugonjwa corona inaendelea kwa Watanzania kuelezwa namna ya kujikinga na ugonjwa huo.



Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Selemani Mzee (kulia), akikata utepe kuashiria kukakabidhi gari jipya la kubeba wagonjwa ambalo limetolewa na Rai John Magufuli, kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Nagaga, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara.**PICHA: HAMISI NASIRI.**

# Waandishi wa Kenya wakamatwa Arusha

**Na Allan Isack, LONGIDO**

WAANDISHI wawili Rai wa Kenya, wanashikiliwa na jeshi la polisi wilayani Longido, mkoani Arusha kwa tuhuma za kuingia nchini bila kufuata utaratibu na kufanya mahojiano na wananchi kuhusu ugonjwa wa Covid-19.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Frenk Mwaisumbe, alisema waandishi hao ambao wote ni wa jinsia ya kiume walikamatwa wakifanya mahojiano na wananchi bila ya kuwa na kibali cha Mamlaka ya Mawasiliano nchini (TCRA).

"Tunatambua kuwa chombo hicho cha habari hakijasajiliwa hapa nchini ,hivyo walitakiwa kupata kibali cha kufanya mahojiano na mamlaka husika ya Tanzania," alisema Mwaisumbe.

Mwaisumbe alisema waandishi wote wananatoka katika televisheni ya elimu "Elimu Tv".

"Waandishi hawa walikamatwa majira ya saa 1:300 wakiwa na vifaa vyao vya kazi huku Longido wakizungumza na wananchi kuhusiana na ugonjwa wa corona," aliongeza Mwaisumbe.

Aidha, alisema baada ya kuwahoji waandishi hao walisema kuwa wametoka nchini kwao, kuja Tanzania kwa ajili ya kufanya mahojiano na wananchi wa eneo hilo kuhusiana na maambukizo ya ugonjwa wa corona.

Mwaisumbe alisema upelelezi ukikamilika waandishi hao watafikishwa mahakamani.

"Naomba vyombo vya habari vya nje ya nchi wanapoingia Tanzania wafuate utaratibu wa kupata vibali vya kuingia na kufanya kazi kwa mamlaka husika," alisema.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, alithibitisha kukamatwa kwa waandishi hao raia wa Kenya.

# Mwanafunzi mbaroni tuhuma mtandao utengenezaji gongo

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

JESHI la Polisi mkoani Rukwa, linawashikiria watu watatu akiwamo mwanafunzi wa darasa la sita kwa tuhuma za kukutwa na mtambo wa kutengenezea pombe haramu aina ya gongo, pamoja na lita 20 za pombe hiyo.

Mwanafunzi huyo mwenye umri wa miaka 19 ni wa Shule ya Msingi Katusa katika Manispaa ya Sumbawanga

Kamanda wa Polisi mkoani Rukwa, Justine Masejo, alisema kuwa watu hao wamekamatwa kufuatia operesheni maalumu iliyoongozwa na mkuu wa upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoani Rukwa, Ralph Meela pamoja na maofisa wa polisi na askari.

Kabla ya kukamatwa kwa watuhumiwa hao, alisema Jeshi la Polisi lilipata taarifa kuwa kuna watu katika kitongoji cha Katusa Manispaa ya Sumbawanga wanafanya biashara haramu ya kuuza gongo, kitendo kinachosababisha mkusanyiko wa watu wanaokunywa pombe hiyo bila kuchukua tahadhari ya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa Covid-19.

Kamanda huyo alisema baada ya taarifa hizo ndipo askari polisi wakiongozwa na Meela walivamia katika eneo hilo na kufanikiwa kuwakamata watuhumiwa hao wakiwa katika eneo la tukio, huku baadhi yao wakiwa wanakunywa pombe hiyo, akiwamo mwanafunzi huyo.

"Baada ya kuwakamata watuhumiwa hao, polisi walibaini kuwa licha ya kutenda kosa la kuuza na kunywa pombe hiyo haramu, hawakuwa wanachukua tahadhari yoyote ya kujikinga kuambukizo ya virusi vya corona kwa kuwa walikuwa katika mkusanyiko... hakuna hata aliyevaa barakoa wala hakuna maji ya kunawa mikono, pia hakuna kitakasa mikono cha aina yoyote," alisema.

Kamanda Masejo alisema watafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

# W'biashara wakumbushwa taratibu, sheria vyuma chakavu

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WATU wasiojulikana wamechoma Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Mtaa wa Ng'ong'ona, Dayosisi ya Dodoma, jijini hapa.

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Sima, amesema ni wajibu wa kila mfanyabiashara wa vyuma chakavu kufuata sheria, ili kulinda miundombinu na kuepuka migogoro.

Sima alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki, alipozungumza na wafanyabiashara hao katika mkutano uliofanyika jijini Tanga na kuwataka kuwa na vibali vya biashara hiyo.

Pamoja na mambo mengine, Naibu Waziri Sima alisema serikali haitawatoza faini kwa mizigo ya vyuma chakavu walizohifadhi na badala yake watatakiwa kuomba vibali upya ili waendelee kufanya biashara.

"Ndugu zangu, hapa tunazumgumzia ule mzigo ulio nao na siyo ule utakaokuwa nao baadaye, maana kuna wengine watafikiri tumesema kuwa hata baadaye ukiwa nao mzigo, hautachajiwa faini, Hapana! Kuanzia sasa kwenye kikao hiki, mtu mwenye mzigo atuambie tufahamu," alisisitiza.

Alisema jukumu la serikali ni kuhakikisha kuwa kila mtu anafuata sheria zilizowekwa huku akitoa rai kwa wafanyabiashara hao kuunda ushirika wa idadi ya watu waliokubaliana kwa pamoja na suala la vibali litakuwa jambo rahisi kwao.

Sima alisema serikali inafanya kazi kwa ukaribu na wafanyabiashara hao, lakini nao wanapaswa kutii maelekezo na kufuata sheria zilizowekwa ili kuepuka migogoro isiyo na ulazima.

"Mwaka 2019, tulitengeneza kanuni, hivyo kila mmoja wetu analazimika kuwa na kibali na sisi tunawajibika kutoa kibali na kama kuna vikwazo katika utoaji wa vibali, tunajadili kwa pamoja wapi tuna tatizo na tunatatua na pia hatuko hapa kuizuia biashara hii," alisema.

Wafanyabiashara hao wakiwasilisha malalamiko yao, walidai kutozwa kiasi cha Sh. milioni 1.5 kwa mwaka, wakidai ni kikubwa tofauti na mitaji yao.

Waliongeza kwa kuahidi kuwa wao kama wananchi, watatekeleza maelekezo ya serikali ya kufanya biashara hiyo kwa kulipia vibali vinavyohitajika bila bugudha yoyote.

Pia, waliahidi kufuata sheria na kuwa jumuiya ya wafanyabiashara watakuwa mabalozi kwa wenzao kuhakikisha wanalipia vibali husika kwa kuwa vibali vinapokuwa rafiki, hakuna haja ya kufanya biashara bila kufuata sheria.

# Madereva malori sasa wagoma kuingia Zambia

**Na Manuel Kaminyoge,**

SONGWE

MADEREVA wa Tanzania wanaoendesha malori wamegoma kuvuka mpakani Tunduma mkoani Songwe kuingia Zambia kwa muda usiojulikana, kwa madai wamechoshwa na ahadi zisizotekelezeka za muda mrefu kuhusu utatuzi wa malalamiko yao ya kunyanyaswa na maofisa wa Zambia.

Wakitoa tamko hilo mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Momba, walisema wamekuwa wakipata manyanyaso makubwa wanapokuwa Zambia, hivyo wameamua wasitishe safari ili kushinikiza mabadiliko kwa maofisa wa Zambia.

Walimuomba mkuu wa wilaya kuwasiliana na serikali ya Zambia kumaliza changamoto hizo ili waendelee kuvusha magari, vinginevyo hawatavuka kutokana na manyanyaso hayo, ambayo wakati mwingine yanahatarisha usalama wa maisha yao.

Dicksoni Jumbe, alisema licha ya kuwa wamekuwa wakifikisha malalamiko yao ngazi mbalimbali, lakini wamekuwa wakiahidiwa kuyashughulikia bila mafanikio.

Alisema kutokana na hali hiyo, wamefikia uamuzi huo na kusisitiza kuwa hawatavusha gari mpaka serikali ya Zambia itakapotatua changamoto hizo.

Aidha, alitaja baadhi ya manyanyaso ni kunyang'anywa pasi za kusafiria, kuwataka wapaki magari ya porini badala ya kwenye miji na kufanywa mradi na askari wa usalama barabarani kwa kuwataka watoe fedha kulipia usafi wa mazingira kila unapoingia wilaya nyingine.

Pia wanalalamikia kuwekwa kalantini siku zaidi ya 20 tofauti na utaratibu wa nchi nyingine wa siku 14.

"Sisi hatuvushi magari yetu mpaka serikali ya Zambia irekebishe hizi kasoro... tumechoka na haya manyanyaso, mpaka wakati mwingine tunatamani serikali ya Tanzania ikamilishe mpaka wake Congo kupitia Sumbawanga," alisema na kuendelea:

.John Mtibani, alisema kwa hali waliyofikia Wazambia ni ukiukwaji wa haki za binadamu kwani dereva anapobeba petroli halafu anaambiwa akapaki porini ni kuhatalisha maisha yake.

Juma Said Irando, Mkuu wa Wilaya ya Momba, alisema kuwa amepokea kilio hicho cha madereva na kuwaahidi kuyafanyia kazi yote waliyoyataja, huku aliwaomba kutositisha huduma kabisa badala yake waendelee kuvusha magari wakati serikali za Zambia na Tanzania zinashughulikia kero hizo.

Irando aliongeza kuwa mewasiliana na Balozi wa Tanzania nchini Zambia na tuko barabarani kufuatilia suala hilo.

"Nawaomba ndugu zangu wakati tunaendelea na mazungumzo pande zote mbili vusheni magari... nina uhakika masuala yenu yote yamezingatiwa na yatashughulikiwa nawaombeni sana," alisema Irando.




Askofu wa Kanisa la KKKT Dayosisi ya Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria, Dk. Emmanuel Joseph Makala (katikati), akimkabidhi Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ushetu, Michael Matomora (aliyevaa shati ya kitenge), ndoo ya maji ya kunawia, sabuni na vitakasa mikono kwa ajili ya waganga wa tiba asili na Kituo cha Ukume vyenye thamani ya Sh. milioni 3. **PICHA: SHABAN NJIA.**

# Miaka 60 jela kwa kumbaka, kumpa mimba mwanafunzi

**Na Jumbe Ismailly,**

SINGIDA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Singida, imemhukumu kutumikia adhabu ya kifungo cha jumla ya miaka 60 jela mkazi wa Kijiji cha Mpipiti, Kata ya Mudida, Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Abduli Bakari (27), baada ya kupatikana na hatia ya kumbaka na kumpa mimba mwanafunzi wa kidato cha pili.

Mwendesha Mashitaka wa Serikali, Elizabeth Barabara, alidai kwamba katika siku siku isiyojulikana Februari, mwaka jana, mshitakiwa alimbaka mwanafunzi mwenye umri wa miaka 15 anayesoma kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Mudida.

Mwendesha Mashtaka huyo alidai pia kwamba huku akijua kwamba binti huyo ni mwanafunzi, mshitakiwa amekuwa akimlaghai mwanafunzi huyo kwa kumpa fedha pamoja na kumnunulia mahitaji mbalimbali ili kumshawishi kufanyanaye tendo la ndoa.

Hata hivyo, baada ya kusomewa shitaka hilo mshitakiwa alikana na ndipo upande wa mashitaka ulipeleka mashahidi watano mahakamani, ambao walitoa ushahidi ulioithibitishia mahakama hiyo bila kuacha shaka yoyote kwamba mshitakiwa ndiye aliyembaka mwanafunzi huyo.

Katika shitaka la pili, ilidaiwa na Mwendesha Mashitaka huyo kuwa katika siku isiyojulikana Februari, mwaka jana mshitakiwa huyo alimpa mimba mwanafunzi huyo (jina limehifadhiwa) mwenye umri wa miaka 15.

Barabara alidai pia kwamba huku akijua kwamba binti huyo ni mwanafunzi, alimpa mimba.

Baada ya kusomewa shitaka hilo, mshtakiwa alikana lakini mashahidi watano walitoa ushahidi uliothibitishia mahakama bila kutia kuacha shaka yoyote kwamba mshitakiwa ndiye aliyempa mimba mwanafunzi huyo.

Kabla ya kutoa hukumu ya kesi hiyo ya jinai namba 230/2019, Hakimu Mfawidhi, Robert Oguda, alisema matukio ya vitendo vya ubakaji na mimba katika wilaya ya Singida vimekithiri sana, hali inayochangia mabinti wadogo kupoteza masomo yao bila sababu zozote za msingi.

Akitoa hukumu hiyo, Oguda alisema kwamba ili liwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia kama ya mshtakiwa huyo, anamhukumu mshitakiwa kwenda kutumikia adhabu ya miaka 30 jela kwa kosa la kwanza la kubaka na katika shitaka la pili la kumpa mimba, alimhukumu pia kifungo cha miaka 30 jela, na makosa yote yanaenda kwa pamoja.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Soka la Tanzania linahitaji wachezaji wa kigeni zaidi

**KUTOKANA** na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona (COVID-19), mkutano uliokuwa ukitarajiwa kuwakutanisha wadau wa soka nchini ili kujadili na kisha kupata muafaka wa hatma ya idadi ya wachezaji wa kigeni nchini, hautakuwapo tena.

Kufanyika kwa mkutano huo ilikuwa ni agizo la serikali kupitia kwa wizara husika ya michezo ambayo kwa maoni ya Waziri wake, Dk. Harrison Mwakyembe anaamini idadi ya wachezaji 10 wa kigeni wanaoruhusiwa kwa sasa ni kubwa, hivyo inapaswa kupunguzwa.

Hata hivyo, kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona vilivyosababisha serikali kupiga marufuku shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu, sasa mjadala huo utafanyika kwa kupitia mtandao wa Baraza la Michezo Tanzania (BMT) kwa kila mdau kutoa maoni yake.

Tunapongeza hatua hii ya serikali ya kutoingilia moja kwa moja kufanya uamuzi katika shughuli za michezo na badala yake kuwaachia wadau kujiamulia. Hivyo, ni wakati wa wadau wa soka kutumia fursa hii adhimu kutoa maoni yao sasa ili uamuzi ukifanyika uwe wa wote badala ya kukaa kimya na kisha baadaye kuanza kulalamika kwa umuazi utakaofikiwa.

Kwa mujibu wa maoni ya Waziri Mwakyembe kama ilivyo kwa baadhi ya wadau wachache wa soka, wanaamini uwapo wa wachezaji wengi wa kigeni unaua vipaji vya wazawa hivyo kuidumaza timu ya Taifa, Taifa Stars jambo ambalo Nipashe kamwe hatuwezi kukubaliana naye.

Tukiwa kama wadau namba moja wa soka nchini, tunaamini wachezaji wa kigeni wanapaswa kubaki 10 kama ilivyo sasa ama kuongezwa na si kuwapunguza, kwani ndiyo wanaowafanya wazawa kuongeza juhudi kwa kupigania namba uwanjani, na si hili la kutaka kuwarahisishia nafasi ya kucheza.

Hiyo ni kutokana na ukweli kwamba; kwanza klabu zenye uwezo wa kusajili wachezaji 10 wakigeni sana sana ni tatu, Simba, Yanga na Azam FC na bado katika vikosi vyao vya kwanza kuna wazawa wengi wanaotoa ushindani wa namba na kupata nafasi, jambo ambalo limewafanya kuwa bora hata kwenye timu ya taifa.

Pili mara nyingi tumekuwa tukipiga kelele wachezaji wetu kuonyesha uwezo na kutafuta nafasi ya kwenda kucheza soka la kulipwa ili kuwa na nyota wengi katika timu ya Taifa, lakini imekuwa vigumu kwao kuweza kupata timu kubwa nje, hivyo hawa wageni wanaotoka nje ndiyo wanaoweza wazawa kuwa bora humu humu nchini.


Kwa mantiki hiyo, kinachotakiwa ni TFF kuhakikisha wachezaji wa kigeni wanaokuja kucheza soka nchini wanakidhi vigezo watakavyoviweka hususan viwango vitakavyoweza kutoa changamoto kwa wazawa kujiimarisha, lingine labda kuweka kanuni ya idadi ya watakaoruhusiwa kucheza katika mechi moja.

Lakini pia kwa wadau wanaotaka wachezaji wa kigeni wanaosajiliwa na klabu nchini kupunguzwa kutoka 10 wa sasa, kama ukitazama Ligi Kuu ambayo msimu ujao itashirikisha timu 16 huku kanuni ikiruhusu kila klabu kusajili jumla ya wachezaji wasiozidi 30, hiyo inamaana jumla yao watakuwa 480, ukitoa 30 wa kigeni kutoka Simba, Yanga na Azam unaweza kufanya 50 wengine wa kigeni ni kutoka klabu zingine 13 na kufanya jumla ya wageni kuwa 80.

Kwa mantiki hiyo wazawa watakuwa 400, hivyo ni vipi wachezaji 80 wa kigeni wazuie wenyeji 400 kuonyesha uwezo wao? Hata hivyo, idadi hiyo ya 'mapro' 80 ni makadrio ya juu sana kwani hata wakati huu Ligi Kuu ikishirikisha klabu 20 bado wageni hawajafikia 80, hivyo kuendelea kuzuia wageni ni kuwalemaza wazawa kwa kuwafanya washindwe kujituma kwa kupigania namba.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Kanuni hizi ni maalum kwa kuzibana Simba na Yanga

**BARAZA** la Michezo la Taifa (BMT) limeanza kupokea maoni kutoka kwa wadau wa soka kuhusu idadi ya wachezaji wa kigeni kwenye soka la Tanzania.

Mjadala huu umekuwa mkubwa sana kwa sasa kwenye redio, televisheni, mitandao ya kijamii na hata mitaani. Kwa sasa kila kona ya nchi mashabiki wa soka wamekuwa wakilijadili suala hili. Na kwa sababu kwa sasa ligi imesimama, basi suala kubwa linalojadiliwa ni hili.

Kumekuwa na dhana kuwa wachezaji 10 wa kigeni ni wengi sana, hivyo baadhi wamekuwa na mpango wa kutaka kuwapunguza na kubaki watano.

Sababu mbalimbali zimekuwa zikitolewa, zikiwamo kuwa wachezaji wa kigeni wanawabana wachezaji wazawa kuonekana au kuonyesha vipaji vyao kiasi kwamba wanaifanya hata timu ya Taifa, Taifa Stars kutokuwa imara.

Mimi binafsi mchango wangu kwa BMT ni huu hapa. Kusema kweli kitendo cha wadau wa soka nchi nzima kuweka mjadala kwa sababu ya wachezaji 10 tu wa kigeni ambao wanasajiliwa na klabu za Simba, Yanga na Azam ni sawa na kuwatengenezea bomu wachezaji wetu.

Ni kuwadekeza na kuwaendekeza. Wachezaji wa Tanzania wanatakiwa wapambane ili wapate namba mbele ya wageni na wasitengenezewe mazingira mepesi. Hapo ndiyo tutawaharibu kabisa.

Kanuni yoyote ile itakayokuja ya kupunguza wachezaji wa kigeni, itakuwa ni ya kuzibana tu Simba, Yanga na Azam.

Maana ya kanuni ni kuzibana klabu zote na si baadhi ili kuzinufaisha zingine. Tanzania tujikite kwenye hoja ya kuzifanya Ndanda, Mbeya City, Mtibwa Sugar kuwa kama Simba, Yanga na Azam na si Simba, Yanga na Azam tuzibane na kuzilazimisha ziwe na uwezo sawa na Ndanda, Biashara United na Mwadui FC.

Timu zingine hazisajili kabisa wachezaji wa kigeni. Zingine zinasajili chini ya watano, hivyo kanuni hiyo ikiwekwa wala haitawagusa.

Hapa ni kuziondolea klabu za Simba, Yanga na Azam nafasi ya kupambana, si kwenye ligi tu, bali hata kwenye mechi za kimataifa. Wala tusidanganyane, Simba, Yanga na Azam ambazo angalau zimekuwa zikifanya vizuri kwenye mechi za kimataifa, ni kwa sababu zina baadhi ya wachezaji wa kimataifa, na timu zingine kama Mtibwa Sugar ambayo msimu uliyopita ilifungwa mechi zote mbili za Kombe la Shirikisho dhidi ya KCCA ya Uganda mabao 5-1 kwa sababu haikuwa na mchezaji wa kigeni hata mmoja.

Kuhusu timu ya taifa, itakuwa ni ajabu kwa nchi kama Tanzania kutegemea wachezaji wa Taifa Stars iti watoke Simba, Yanga na Azam tu. Katika soka la Afrika kwa sasa, karibuni nchi zote zinategemea zaidi wachezaji kutoka nje ya nchi.

Hata Madagascar ambayo ilitesa msimu huu kwenye AFCON, ilikuwa na wachezaji wengi kutoka Ufaransa, tena wa madaraja ya chini, lakini walikuja kufanya vema kwenye timu ya taifa.

Hivi kweli tunashindwa hata na Madagascar? Tunachotakiwa Watanzania ni kuwatengeneza wachezaji vijana na kuwatawanya waende nchi mbalimbali kucheza soka la kulipwa, lakini pia wachezaji wa klabu mbalimbali nao watoke wapishane na wageni, waende nje ili waitwe kucheza timu ya taifa.

Tunahitaji Taifa Stars iwe na wachezaji wengi kutoka nje ya nchi, Simba, Yanga, Azam, au KMC na zingine wachangie wawili, watatu au mmoja.

Haiwezekani nchi kama hii itegemee wachezaji wengi wa Stars kutoka timu hizo tu, wakati Senegal wao wanaita wote kutoka Ulaya, hata wanaocheza Afrika huwa hawaitwi. Tuziache Simba, Yanga na Azam na wachezaji wao 10 kwa sababu nazo zina mahitaji yao, wanahitaji siku moja watwae Kombe la Ligi ya Mabingwa Afrika au Shirikisho na hilo huwezi kulipata kwa kuwa na wachezaji wa Kitanzania waliorahisishiwa kucheza kwa kusaidiwa na kanuni na si uwezo.

Labda tunaweza kukubali kwa mbali kuwa wachezaji hao 10, iwekwe kanuni kuwa wawe wanacheza watano tu wa kigeni kwenye kila mechi moja.

HABARI KITAIFA



Mkuu wa Mafunzo na Utendaji Kivita wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Meja Jenerali Alfred Kapinga, akiangalia kifaa cha kupimia mwelekeo wa Mzinga wakati wa zoezi maliza kwa ajili ya Kuruta kundi la 39 wa shule ya mafunzo Kihangaiko. **PICHA: LUTENI SELEMANI SEMUNYU**.

# Waziri agiza wadaiwa sugu kufikishwa mahakamani

**Na Francis Godwin,** IRINGA

NAIBU Waziri Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, ameiagiza Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, kuwaandikia barua wadaiwa sugu wa kodi ya ardhi ili kulipa ndani ya mwezi mmoja ama kufikishwa mahakamani.

Akizungumza jana wakati wa ziara yake mkoani Iringa Naibu Waziri huyo, alisema kuwa lazima halmashauri hiyo na nyingine nchini kuhakikisha zinawabana wadaiwa sugu wa kodi za ardhi, ili walipe kwa wakati badala ya kuendelea kuwafumbia macho.

"Kuwa kuanzia leo wadaiwa wote wa ardhi wanapaswa kuandikiwa barua za kukumbushwa kulipa madeni yao ndani ya mwezi huu na kama wasipofanya hivyo basi kufikishwa katika mahakama ya ardhi ili sheria ichukue mkondo wake .

Aidha, Naibu Waziri huyo alisema zimekuwepo sababu kwa baadhi ya Halmashauri kusingizia kushindwa kufuatilia ukusanyaji wa kodi za ardhi kwa madai ya janga na virusi vya Corona, jambo ambalo si kweli kwani ukusanyaji wa kodi unaweza kuendelea kama kawaida na Corona isiwe sababu ya watumishi kukwepa majukumu yao ya utendaji .

"Mbona hapa tumeweza kukutana na kufanya ziara hii sasa ninyi mnashindwa vipi kupita mitaani kuwakumbusha wananchi wanaodaiwa kodi za ardhi kulipa kodi hizo na njia za kutumia mnazo nyingi hapa mnazo radio za kijamii na vyombo vingine vya habari pamoja na magari ya kuzunguka kufanya matangazo tumieni njia hizo kuwafikishia wananchi ujumbe," alisema.

# DC awasihi walimu kujilinda na corona

**Na Gideon Mwakanosya,** MBINGA

MKUU wa Wilaya ya Mbinga, Cosmas Msheni, amewataka walimu kuchukua tahadhari dhidi ya maambukizo ya ugonjwa wa corona.

Aidha, amewapongeza walimu kwa ufaulu mzuri wa wanafunzi kwa kipindi cha mwaka 2019/2020.

Msheni ametoa tahadhari hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano mkuu wa uchaguzi wa walimu wa wilaya ya Mbinga, uliofanyika mjini hapa na kuhudhuriwa na zaidi ya walimu 280.

Alisema kuwa walimu wa wilaya hiyo wanastahili pongezi kwa kuwa matokeo ya mtihani wa taifa wa darasa la saba, mtihani wa taifa wa kidato cha nne na cha sita yalikuwa mazuri tofauti na matokeo ya wilaya nyingine mkoani humo.

Alieleza zaidi kuwa ni vyema walimu wote wa wilaya hiyo kuwa mabalozi wazuri wakutoa elimu ya ugonjwa wa corona kwa wanafunzi wao pamoja na wananchi kwa leo la kuwa na tahadhari ya ugonjwa wa corona.

Naye, Katibu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Wilaya ya Mbinga, Peter Simwanza, alisema kazi kubwa ya chama hicho ni kuhakikisha kuwa walimu wanapofanya kazi zao za kufundisha wanapaswa kuwa waadilifu kwa kuzingatia ufundishaji bora kwa wanafunzi wao.

Kwenye mkutano huo msimamizi wa uchaguzi Bernard Mbawala, alimtangaza Nicodem Hyera kuwa Mwenyekiti mpya wa CWT wa Wilaya ya Mbinga kwa muda wa miaka mitano.

Washindi wengine kuwa ni Grace Mbele ambaye ameshinda nafasi ya mweka hazina, mwakilishi wa walimu wanawake Winfrida Mbata, Hekelius Ndunguru, mwakilishi wa kundi la walimu wenye ulemavu na Lenzile Malena kuwa mwakilishi wa kundi la vijana.

# Watanzania watakiwa kutembelea vivutio

**Na Daniel Sabuni,** SERENGETI.

WATANZANIA wametakiwa kujenga utamaduni wa kutembelea hifadhi za taifa na kufurahia urithi wa vivutio pamoja na kuchangia pato la Taifa.

Hatua hiyo itasaidia watalii wa nje wanapoahirisha safari nchi iendelee kupata mapato yatokanayo na utalii kwa maendeleo yao.

Mkuu wa Kitengo cha Utalii wa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti,Tutinaga Mwakijambile, aliyasema hayo juzi alipozungumza na Nipashe kuhusu masuala mbalimbali ya utalii.

Alisema ni vyema ikafikia wakati Watanzania kuamua kutembelea hifadhi za Taifa kama watalii wa ndani badala ya kutegemea wa nje pekee.

"Hifadhi hizi na vivutio vilivyomo ni mali ya Watanzania, niwaalike Watanzania kuja Serengeti wafurahie Hifadhi hii ambayo ni moja ya maajabu yaliyopo duniani...wataweza, wadundulize pesa halafu waungane kwenye vikundi, ushahidi ni kwamba hata watalii wa nje wanafanya hivyo," alisema Mwakijambile.

Alitaja vivutio vinavyopatikana Senapa ni wanyama wanaohama kutoka Tanzania na kuelekea Masai Mara nchini Kenya kila mwaka, makundi makubwa ya simba, tembo, mbwamwitu, muonekano wa uwanda mpana usio na mwisho kwa upeo wa macho, makundi ya twiga, mbuni, swala pala, viboko, chui, duma, pimbi, faru, nyati, mito mikubwa ya Grumet na Mara ambayo inatiririsha maji hifadhini na kivutio cha kuruka na puto.

Vivutio vingine vinavyovuta watalii wengi Serengeti ni wanyama maarufu 5 duniani wanaonekana kwa wingi.

Mwakijambile alitaja kivutio kingine kinachovuta watalii ni wanyama aina ya nyumbu wanaokadiriwa kufika milioni moja na nusu( 1.5 milioni) ambao huchunga kwenye eneo moja na kubeba mimba kwa wakati mmoja maalum, kuzaa kwa wakati, kulea kwa wakati na safari ya kuhama kwa pamoja kwenda upande mwingine wa Masai Mara kutafuta malisho na maji safi.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, akimsikiliza Mtaalamu Mshauri wa Mradi wa Kurasimisha Ardhi Vijijini unaotekelezwa na Shirika la Feed the Future, Malaki Msigwa (kulia), alipotembelea Masijala ya Ardhi ya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, wakati wa ziara yake mwisho mwa wiki. Habari Uk. 7. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watumishi watatu H/Itigi wafukuzwa kazi

**Na Jumbe Ismailly,** ITIGI

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Itigi, wilayani Manyoni, mkoani Singida, limewafukuza kazi watumishi watatu wa Halmashauri hiyo, akiwemo Daktari Msaidizi daraja la kwanza, Zuberi Hamisi Abdala, baada ya kupatikana na makosa ya kughushi vyeti vya kidato cha nne.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Itigi, Ally Minja, aliwataja watumishi waliofukuzwa kazi kwa makosa ya kuwa na vyeti vya kughushi, kuwa ni Mhandisi daraja la pili, Shabani Mughu aliyekuwa na kosa la kughushi cheti cha uhandisi.

"Kulikuwa na hoja ya kukamilisha mchakato wa watumishi ambao waliondolewa utumishi kwa makosa ya kuwa na vyeti vya kughushi," alifafanua Mwenyekiti Minja.

Wengine ni Zuberi Abdallah, aliyekuwa Daktari Msaidizi daraja la kwanza aliyepatikana na kosa la kughushi cheti cha kidato cha nne na Sophia Richard, muuguzi daraja la pili aliyegushi pia cheti cha kidato cha nne.

"Katika kikao cha leo tulileteva mashitaka matatu na baraza limekubaliana na kukubali kwamba hawa watumishi wote watatu wamefukuzwa kazi kuanzia leo," alifafanua Minja.

Aidha, Minja aliweka wazi pia kwamba baraza hilo pia limewathibitisha kazini watumishi wapatao saba wa idara ya utawala baada ya kutimiza vigezo vya kuwa kazini kwa muda wa mwaka mmoja na kutopatikana na dosari yeyote ile katika kipindi hicho.

Minja ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Itigi aliwataja waliothibitishwa kazini kuwa ni Ofisa Mtendaji wa kata ya Itigi mjini, Simoni Tililo, Afisa Mtendaji wa kata ya Aghondi, Nuru Maulidi, Afisa Mtendaji wa kata ya Idodyandole, Thomasi Sebastiani, Ofisa Mtendaji wa Itigi Majengo, Athumani Mkwawa, Ofisa Mtendaji wa kata ya Mitundu, Rashidi Masudi, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Tambukareli, Ibrahimu Ntandu na Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mwamagenbe, Zuhura Kipehi..

# Asimulia alivyonusurika mdomoni mwa chatu

**Na Said Hamdani,** LINDI

KIJANA Hatibu Malilo (23) wa Mtaa wa Angaza, Kata ya Wailes, Manispaa ya Lindi, amenusurika kufa baada ya kushambuliwa na nyoka aina ya chatu, alipokuwa akichunga ng'ombe.

Akizungumza na Nipashe jana, alisema mkasa huo ulimpata Mei 04 mwaka huu, majira ya saa 9:00 alasiri eneo la Angaza iliyopo shule ya Sekondari.

Akisimulia tukio hilo alisema kuwa, alikiwa na mwenzake Hamisi na Said, alishambuliwa na chatu huyo ambaye alibanwa miguu yote.

Alisema wakati amezingirwa na nyoka huyo, Malilo alishindwa kuendelea na safari yake kwa kile alichokielezea miguu ilikuwa mizito na alipojiangalia alibaini ameshikwa na mnyama huyo na kupiga kelele kuomba msaada kutoka kwa wenzake aliokuwa ameongozana nao.

Mchungaji huyo alisema wakati akiomba msaada huo ng'ombe aliokuwa nao alimfuata na alipokaribia eneo hilo na kunusa, akawa anafokewa na Chatu huyo, hali iliyomfanya aondoke na kufuata wenzake.

"Chatu yule baada ya kunishika miguu niliishiwa nguvu ikizingatiwa sikuwa na silaha kali kama vile kisu au panga, hivyo nikawa napiga kelele kuomba msaada kutoka kwa wenzangu," alifafanua Hassani.

Alisema wakati akiwa tayari amezidiwa nguvu kisha kuangushwa chini na chatu huyo wenzake walifika eneo la tukio na kufanikiwa kumuokoa kwa kumshambulia nyoka kwa mawe, na kufanikiwa kumuachia na kutokomea msituni huku akibaki hajitambui na kuishiwa nguvu.

Malilo alisema baada ya nyoka yule kumuachia wachungaji wenzake walimbeba na kumfikisha nyumbani kwao na kupata fahamu baada ya zaidi ya saa matatu, kufuatiwa jitihada zilizofanywa na watoa msaada, ikiwamo kufanyiwa dawa za asili. Alisema kukamatwa kwake na chatu huyo anayekadiliwa kuwa na urefu usiopungua futi 10 kulichangiwa na ng'ombe mmoja kati ya kumi aliokuwa anachunga kumtoroka kuelekea eneo la bondeni.

"Nitachukua muda kuniondoka nyoka huyu kichwani mwangu kwani ni mara yangu ya kwanza kunipata mtihani wa aina hii," alisema Hassani.

Kwa upande wake, mmiliki wa ng'ombe hao, Husuna Kalua, akizungumzia mkasa huo, alisema anamshukuru Mungu kwa kijana huyo kunusurika.

# Ofisa elimu awaonya walimu wafundisha tuisheni

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

OFISA Elimu mkoani Kigoma, Majuto Njunga, amewataka wazazi kuacha kukiuka maagizo ya Serikali kwa kukusanya makundi ya watoto na kuwatafutia walimu wa kuwafundisha wakiwa ndani, jambo linalowaweka hatarini kuambukizwa corona.

Katibu Tawala Mkoa wa Kigoma, Rashid Mchata, aliyasema hayo jana wakati wa kukabidhi vifaa vya kujikinga na maambukizo Corona vilivyolotewa na Shirika la Compassion Of Afica kupitia muungano wa makanisa 12 linalohudumia watoto 2,718, wanawake wakiwa 1384 wanaume 1334 katika Manispaa ya Kigoma Ujiji.

Alisema kuna taarifa zenye uhakika kuwa kuna makundi ya watoto yanafungiwa ndani na kufundishwa masomo wakati, Serikali imepinga jambo hilo ili kuwaweka watoto salama.

"Niwaombe wazazi msitumie nyumba zenu kama twisheni kwani mnahatarisha usalama wa familia zenu na kukiuka agizo la serikali la kuwaondoa watoto katika hatari ya kuambukizwa ugonjwa wa corona," alisema.

Aidha, Njunga aliwataka wanafunzi watumie vipindi vya elimu vinavyoendeshwa kupitia runinga na si kutumia walimu ambao Serikali haijawathibitisha katika ufundishaji.

Awali, akizungumza kwa niaba ya wachungaji, Mchungaji Riziki Jacksoni alisema Shirika la Compassion katika kipindi hiki limeendelea kutoa elimu kwa jamii ya namna ya kujikinga pamoja na kufanikiwa kutoa vifaa kinga kama ndoo za koki na vitakasa mikono vyenye thamani ya Sh. milioni 45.472.

Malieta Alex akizungumza kwa niaba ya wazazi baada ya kupokea vifaa hivyo, alisema vitawasaidia kwani tangu kuwepo kwa mlipuko wa ugonjwa wa corona vifaa kinga vimepanda bei na kufanya baadhi ya watu kutokumudu gharama.

## HABARI KITAIFA

# Nemc yaonya umwagaji wa majitaka mitaroni

**Na Mwandishi Wetu**

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (Nemc) limewataka Watanzania, hasa waishio mijini, kuacha kutiririsha majitaka katika mitaro iliyojengwa kusafirisha maji ya mvua.

Baraza limetoa angalizo hilo kwani tabia hiyo inahatarisha afya ya umma na kuharibu mazingira.

Akizungumza jijini Dar es Salaama mwishomi mwa wiki baada ya kutembelea eneo la makazi la Mabibo na Ukanda Maalumu wa Viwanda katika eneo hilo, Mkurugenzi Mkuu wa, Dk Samuel Gwamaka, alisema ameshtushwa kuona wananchi wameelekeza mabomba ya majitaka kutoka majumbani na kumwaga katika mtaro mkubwa wa umma unaosafirisha maji ya mvua hadi Mto Msimbazi na kwenda baharini.

Alisema jambo hilo limemsikitisha sana na kufafanua kwamba kasoro hiyo inahatarisha afya ya wananchi wa Mabibo na wa mbali na kuharibu mazingira. "Wananchi kuelekeza mabomba ya majitaka kwenye mitaro maalumu ya umma siyo matumizi sahihi ya mitaro hiyo ya umma.

"Tunawaonya wananchi wanaofanya hivyo nchini kuacha mara moja tabia hiyo kwani inahatarisha afya ya umma na kuaharibu mazingira," alieleza.

Dk Gwamaka alitembelea eneo la Mabibo baada ya NEMC kupokea barua inayolalamikia kiwanda cha kutengeneza nguo kwa uchafuzi wa mazingira kwa njia ya moshi, kelele na maji yenye kemikali na sumu.

"Jambo hili litafuatiliwa kwa makini kwa kuunda timu ya wataalaamu. Ikibainika kwamba kiwanda chochote kimekiuka matakwa ya Sheria ya Mazingira ya 2004, hatua kali za kisheria zitachukuliwa," alieleza.

Hata hivyo, Dk Gwamaka aliwataka wananchi kuacha tabia ya kunyoshea vidole taasisi au kiwanda huku wao wakiwa mstari wa mbele katika kuharibu mazingira badala ya kuyalinda.

Aliwataka wananchi na viongozi kuelewa kwamba mazingira salama ni muhimu kwa ustawi wa watu, wanyama na viumbe vingine na kuwaomba viongozi wa serikali za mitaa kuhakikisha miundombinu inatumika kwa shughuli tu liliyokusudiwa.

"Mamlaka zote tukisimamia hili tutaepusha madhara kwa wananchi, mifugo na viumbe vingine vilivyomo katika mazingira yetu," alisema.



Mafundi wakiwa kwenye maandalizi ya ujenzi wa tangi la maji Kisarawe-Pugu, Pugu Kajiungeni. Mradi huo unatekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es salaam (DAWASA), tangi hilo litakuwa na uwezo wa kuhifadhi maji yenye ujazo wa lita milioni mbili. **PICHA: FRANK MONYO**

# Madiwani CUF watimkia CCM kumuunga mkono Magufuli

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MADIWANI 9 wa Chama cha Wananchi (CUF) Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, wamejiondoa kwenye chama hicho na kujiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Madiwani waliokihama chama hicho na majina ya kata zao kwenye mabano ni Aloyi Mohmmed Nyoni (Mlingoti Mashariki), Ajolla Hasan Ally (Ligunga), Maganga Husein Zuberi (Nandembo) na Kabago Halifa Sandali (Nalasi Maghalibi).

Wengine ni Kubodola Idrisa Ambali (Nakapanya), Said Ally Pindu (Ngapa), Abdalah Rajab Abdallah (Majengo) , Aliasa Mohammed Mshamu (Tinginya) na Zainabu Mussa Said (Diwani wa viti maalumu Mlingoti Maghalibi).

Sambamba na madiwani hayo pia kiongozi mwandamizi wa chama hicho, Said Kiosa pia ameungana na madiwani hao kwa kuachia nyadhifa zote alizo kuwanazo ndani ya chama hicho na kujiunda na CCM.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti walisema kuwa huo ndiyo uamuzi wao kwa sasa, hasa kwa viongozi waliokomaa kisiasa zikiwa ni juhudi za kuunga mkono juhudi zinazo oneshwa na Rais John Mgufuli.

Walisema Rais Magufuli amefanya mambo mengi kwa kipindi kifupi yakiwamo mambo ambayo viongozi wengi wa kitaifa wa vyama vya upinzani walikuwa wakivilalamikia.

Katibu wa CCM Wilaya ya Tunduru, Kite Mfilinge, pamoja na kuwakaribisha ndani ya chama hicho pia aliwaomba Wanachama na wakereketwa wa CCM kuwapokea wanachama hao wapya, na kwamba wapo huru kugombea nafasi yoyote ndani ya chama.

Akizungumzia tukio hilo, Diwani wa CUF Kata ya Kidodoma, alisema kuwa kitendo cha viongozi waandamizi hao wa CUF kukihama chama hicho na kujiunga CCM kimeonyesha udhaifu mkubwa katika vyama vya upinzani.

# Osha yawawezesha wasioona kujikinga maambukizo corona

**Na Gwamaka Alipipi**

WAKALA wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (Osha), umetoa msaada wa vifaa kinga kwa Chama cha Wasioona Tanzania, ili kuwawezesha kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa virusi vya corona.

Vifaa hivyo vilivyokabidhiwa kwa viongozi wa chama hicho ni vitakasa mikono (sanitizers), barakoa, ndoo za kunawia mikono, pamoja na sabuni za maji.

Akikabidhi vifaa hivyo kwa viongozi wa chama, Kaimu Mtendaji Mkuu wa Osha, Khadija Mwenda, alisema jukuku la Osha ni kuhakikisha maeneo ya kazi yanakuwa salama, kwamba wameguswa na changamoto inayolikabili kundi hilo maalumu katika kujikinga na ugonjwa wa corona.

"Sote tunafahamu kwamba dunia na nchi yetu ipo katika mapambano dhidi ya janga la corona, kila mtu anahimizwa kuchukua tahadhari dhidi ya virusi hatari vya corona kwa kutekeleza maelekezo mbalimbali yanayotolewa na wataalamu wetu wa afya, hivyo kwa kutambua changamoto zinazowakumba wenzetu wasioona tumeona ni vema tukawasaidia baadhi ya vifaa kinga muhimu," alisema Mwenda.

Alisema watu wasioona wanakuwa na wakati mgumu zaidi katika kujikinga na ugonjwa wa corona kutokana na hali yao, na kwamba mara nyingi hulazimika kugusana na watu wengine hata wasiowafahamu hususani wanapohitaji msaada wa kuvushwa barabara au kuongozwa toka eneo moja kwenda lingine.

"Miongoni mwa vifaa tulivyotoa ni vitakasa mikono ambavyo vipo katika chupa ndogo ambazo walengwa wataweza kutembea nazo na hivyo kuwawezesha kutakasa mikono yao kila wanapolazimika kugusana na watu wanaowaongoza au wanapokuwa wameshika vitu mbalimbali," alisema Mwenda.

Aidha, aliwaomba wadau wengine kujitokeza na kutoa misaada zaidi kwa makundi ya watu wenye ulemavu ili nao waweze kujikinga na kuendelea kushiriki katika shughuli mbalimbali za ujenzi wa Taifa.

Kwa upande wake Mratibu wa Idara ya Maendeleo ya Vijana na Chipukizi wa Chama hicho, Omari Itambu, aliwashukuru Osha kwa msaada huo muhimu kwa wanachama wake.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Wasioona Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Zumba, alisema: "Kwa niaba ya wasioona wa mkoa wa Dar es Salaam, tunapenda kuwashukuru Osha kwa msaada huu wa vifaa vya kujikinga na ugonjwa hatari wa corona na tungependa pia kutoa wito kwa watu wengine waweze kutusaidia pia kwani watu tusioona tupo katika hatari kubwa zaidi ya kuambukizwa ugonjwa huu."

# Ataka mahakama udhalilishaji watoto

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

AFISA Ustawi Hifadhi ya Mtoto Wilaya ya Wete, Pemba, Nafhat Salim Yahya, ameishauri Serikali kuanzisha mahakama maalum itakayosikiliza kesi za udhalilishaji pekee, ili zisikilizwe kwa haraka.

Aiidha, ofisa huyo amesema hatua hiyo itasaidia kuharakisha kesi hizo na haki kipatikana haraka.

Akizungumza na Nipashe mjini Wete ofisa huyo alisema kuwa iwapo kesi za udhalilishaji zitasikilizwa na kutolewa maamuzi haraka itasaidia kupunguza vitendo hivyo kwa kiasi kikubwa.

Alisema kuwa, ipo haja ya kuanzishwa mahakama maalum ambayo itasikiliza kesi za udhalilishaji pekee badala ya kuchanganywa na kesi nyengine, jambo ambalo litasaidia kesi kusikilizwa na kupata hatia kwa muda mfupi.

"Hizi kesi za udhalilishaji zinaposikilizwa katika mahakama ambazo pia husikiliza kesi nyingine, husababisha kuzorota na kukaa kwa muda mrefu bila kutolewa hukumu," alisema na kuongeza:

"Lakini iwapo itawekwa mahakama kwa ajili ya kesi hizi tu, basi tutafanikiwa kudhibiti."

Alieleza kuwa ucheleweshwaji wa kutolewa maamuzi kwa kesi hizo kunapelekea jamii kukata tamaa na kuona kwamba haki haitendeki, hivyo ikiwa itakuwapo mahakama maalumu, itasaidia kwa kiasi kikubwa kesi kusikilizwa na kutolewa maamuzi, jambo ambalo jamii itafurahia.

Aidha, ofisa huyo aliziomba mahakama kuweka miundombinu rafiki itakayomsaidia mtoto kutoa ushahidi mzuri bila ya woga.

"Mtoto na mtuhumiwa wanaonana uso kwa uso, hii hupelekea kuwa na hofu na kushindwa kutoa ushahidi vizuri," alisema.

Sheha wa Shehia ya Piki, Assaa Khamis Mussa, aliliomba Jeshi la Polisi kuharakisha upelelezi wa kesi za udhalilishaji, ili zifikishwe mahakamani zipate hatia kwa haraka.

"Kesi zinachelewa upelelezi na zinpofika mahakamani huchelewa kutolewa maamuzi, zinapochelewa jamii huona kama hakuna hatia kwa washtakiwa."

Nae Sheikh Khamis Hamad Nassor, mkaazi wa Shengejuu, alisema pamoja na kuwapo kwa hukumu za kesi hizo, bado baadhi ya kesi zinachelewa kutolewa maamuzi.

"Sijui ni kipi kinachosababisha kesi kutolewa maamuzi, kesi hizi si za kucheleweshwa maana jamii inachoka na watendaji wa makosa wanaendelea kuwadhalilisha watoto," alisema.

Mratibu wa Chama Cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) ofisi za Pemba, Fat-hiya Mussa Said, alisema ni jambo jema iwapo itaanzishwa mahaka maalumu, kwani wana imani kuwa vita dhidi ya vitendo vya udhalilishaji vitafanikiwa.

"Mahakama maalumu kwa ajili ya kesi hizo ni jambo zuri kuwapo, kwani kesi zitapata hatia haraka na kwa muda mfupi," alisema.

Jumla ya kesi 74 zimefikishwa mahakama ya Mkoa Wete kuanzia Januari mwaka 2019 hadi Machi 2020, ambapo kesi 23 zilitolewa hukumu mwaka jana.

# Kanyasu akerwa uvamizi maeneo hifadhi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ameonyesha kukerwa na baadhi ya wananchi wanaoendelea kujenga nyumba na kuendesha shughuli za kilimo katika maeneo yenye wanyamapori hasa katika mapito ya wanyamapori.

Alikerwa na hali hiyo katika eneo la Kwakunchinja linalounganisha Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na Hifadhi ya Manyara.

Alisema kutokana na tabia hiyo, Serikali haiwezi kumaliza kulipa vifuta jasho na vifuta machozi kwa wananchi wanaoshambuliwa na wanyamapori wakali na waharibifu

Aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na viongozi wa Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Burunge (WMA) iliyopo wilaya ya Babati, mkoani Manyara kuona namna ya kulinda ushoroba wa Kwakunchinja ambao ni umuhimu kwa Wanyamapori wanaotoka Hifadhi ya Taifa ya Tarangire kuelekea Hifadhi ya Ziwa Manyara.

Alisema kwa mwaka huu pekee Serikali imetumia kiasi cha Sh. bilioni moja kulipa vifuta jasho na vifuta machozi huku kiasi cha Sh. bilioni 2.3 ikiwa bado hakijalipwa kwa wananchi walioathiriwa na wanyamapori wakali na waharibifu

Alisema kila mahali wananchi wamekuwa wakilalamika kuchelewa kulipwa vifuta jasho na vifuta machozi kutokana na madai hayo kuwa mengi hali inayopelekea Wizara kuwa na madai mengi yasiyolipika kutoka kwa wananchi ambao baadhi wameyafuata makazi ya wanyamapori

Hata hivyo, Kanyasu alisema Serikali inatafuta mbinu mbadala ya kupunguza migogoro kati ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu baada ya kugundua kuwa fidia sio suluhisho kutokana na wimbi kubwa la wananchi kuendesha shughuli za kibinadamu katika shoroba za wanyamapori pamoja na maeneo ya mitawanyiko ya wanyamapori .

Alisema kutokana na tabia ya baadhi ya wananchi kufanya makazi katika maeneo hayo, Wizara ya Maliasili na Utalii imegundua hata ikitenga bajeti nzima ya Wizara kwa ajili ya kulipa vifuta jasho na vifuta machozi haitaweza kumaliza tatizo hilo.

Kanyasu alisema binadamu wamekuwa wakiwafuata Wanyamapori hivyo suala la mazao ya kushambuliwa ni jambo lisiloepukika

“”Sehemu ya Mapori ya Akiba na Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori ndimo wananchi wameanzisha makazi hivi unategemea wanyamapori watulie tu?" alihoji Kanyasu.

Alifafanua kuwa wananchi waliojenga katika maeneo hayo wamekuwa wakitoa visingizio kuwa ardhi imepungua na hivyo kuwalazimu kuanzisha shughuli za binadamu katika maeneo ya wanyamapori suala ambalo ni umekuwa ni mzigo kwa Serikali ya kuanza kulipa fidia kila mwaka.

Alisisitiza kuwa shida sio ardhi bali wananchi wameshindwa kutumia ardhi waliyonayo kimipango hata hivyo Wananchi walio wengi wanataka kufuga mifugo kwa idadi kubwa na sio kwa ubora.

Akizungumzia Kilimo, Mhe.Kanyasu alisema wakulima wamekuwa wakilima kizamani kwa kuamini kulima eneo kubwa ndio kupata mazao mengi jambo ambalo si kweli.



Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe (kushoto), akizungumza na Mkuu wa Idara ya M-Pesa Biashara wa Vodacom Tanzania, Happiness Shuma, wakati wa uzinduzi wa majaribio ya mfumo wa ukataji tiketi za mabasi ya kwenda mikoani kwa njia ya mtandao uliozinduliwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini ( LATRA) jijini Dar es Salaam. Katikati ni Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Gilliard Ngewe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Watoto wa mazingira magumu wapewa vifaa ili kujikinga corona

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA.

WATOTO wanaoishi katika mazingira magumu katika mitaa mbalimbali iliyopo jijini Mwanza, wamepewa elimu pamoja na msaada wa vifaa vya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa COVID-19 unaosababishwa na virusi vya corona.

Uwezeshaji huo umefanywana shirika lisilo la kiserikali la Watoto Wema Tanzania Foundation.

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada wa vitakasa mikono, barakoa na groves za mkononi kwa watoto hao, Mkurugenzi wa shirika hilo, Jose Mtuki, alisema lengo ni kuwafikia watoto wengi zaidi waishio katika mazingira magumujJijini Mwanza, kwa kutoa vifaa na elimu ya namna ya kujikinga na maambukizo ya virusi hivyo sambamba na kuunga mkono jitihada za serikali katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

Alisema katika kipindi hiki ni vyema kuwafikia watoto hao, huku lengo lao ni kufikia watoto 20,00,000 ili kupukana na mikusanyiko kila jumamosi watapita kila mtaa nakugawa bidhaa hizo .

"Zoezi ili litakuwa endelevu hadi mambo watakapokuwa sawa vifaa tutakuwa navyo tutakapokuwa tunapita mitaani tukimkuta mtoto yeyote tutamgawia na kumuelimisha hapohapo," alisema Mtuki.

Dan Kitambala, mwalimu Shule ya Sekondari ya Wavulana Bwiru na Erick Michael ambaye ni mwanafunzi wa Kujitolea Shule ya Sekondari Mwanza wakitoa elimu kwa watoto hao, waliwataka kujitenga na mikusanyiko isiyo na kutopiga chafya hovyo ili kutowaathiri wengine.

Naye Baraka Deus, mmoja wa watoto wa mitaani akizungumza kwa niaba ya wenzake baada ya kupokea vifaa hivyo, alisema wanalishukuru shirika hilo kwa kuonyesha umuhimu wao na kuwakumbuka hivyo watazingatia maelekezo na elimu yote ya kujilinda kama waliyovyopewa.

Nipashe
Spotika



MAKOCHA 5 BORA WASIO NA KAZI NA KLABU ZINAZOWAFAA UK. 12&13



# MASTRAIKA WA5 WAKALI WA PASI ZA MWISHO EPL

ROONEY

**LONDON,** England

WASHAMBULIAJI wa daraja la juu mara zote wamekuwa kwenye uhitaji mkubwa hasa kwenye ligi zenye ushindani mkubwa kama Ligi Kuu ya England. Kutoka kwenye kuwa wachezaji wanaolipwa mishahara mikubwa, washambuliaji hao mara zote wamekuwa wachezaji muhimu zaidi kwenye timu.

Ingawa washambuliaji hawa kazi yao kubwa ni kufunga mabao na kuipa timu ushindi, wengine wameonekana kuwa na ujuzi mwingine nje ya kufunga mabao. Kwa miongo mitatu tangu kuanza kwa zama mpya za Ligi Kuu ya England, kumekuwa na mastraika ambao ni mabingwa wa pasi za mwisho 'asists'. Hivyo, hapa tunawaangalia mastraika watano wakali wa 'asisti' katika historia ya Ligi Kuu England.

### 5. ANDY COLE – ASISTI 73

Andrew Cole akiwa pale Manchester United, alikuwa anaitwa mashine ya kufunga mabao wakati wake kwenye Ligi Kuu ya England.

Uwezo wake mkubwa wa kufunga mabao unajulikana. Mabao 187 ni ushahidi tosha, lakini pia anashika nafasi ya tano kwa kuwa mchezaji mwenye asisti nyingi zaidi kwenye ligi hiyo kwenye klabu yake.

Safari ya kucheza kwenye klabu saba tofauti kwenye Ligi Kuu kumemfanya kufikisha jumla ya asisti 73 katika klabu za Newcastle United, Manchester United, Blackburn Rovers, Manchester City na Portsmouth.

### 4. THIERRY HENRY – ASISTI 74

Thierry Henry anashikilia rekodi ya kuwa na asisti nyingi zaidi kwenye msimu mmoja wa ligi, wakati alipofikisha 20 msimu wa 2002-03 katika kikosi cha Arsenal. Raia huyo wa Ufaransa, pia alifunga mabao 24 msimu huo.

Mfaransa huyo ana asisti 74 pamoja na rekodi ya kushinda Kiatu cha Dhahabu mara nne kwa jina lake. Pamoja na kiwango cha mafanikio alichokipata kwenye Ligi Kuu ya England akiwa na Arsenal, Barcelona kule Hispania na timu ya Taifa ya Ufaransa, anabakia kuwa mchezaji wa daraja la juu ambaye hajawahi kushinda tuzo ya Ballon d'Or.

### 3. TEDDY SHERINGHAM – ASISTI 76

Mkali mwingine wa Manchester United kwenye orodha hii, na jina lake ni Teddy Sheringham. Sheringham alitua Old Trafford kipindi cha majira ya joto mwaka 1997 kuvaa viatu vya Eric Cantona aliyekuwa anaondoka. Licha ya kuanza taratibu, Sheringham alikuja kuwa na mafanikio makubwa.

Akiwa hajashinda chochote kwenye kipindi chake cha uchezaji kabla ya msimu wa 1998-99, ambapo Sheringham alishinda mataji ya Ligi Kuu, Ligi ya Mabingwa Ulaya na FA - na kuingia kwenye kitabu cha historia.

Alionyesha uwezo mkubwa kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati wakitoka nyuma na kushinda dhidi ya Bayern Munich. Sheringham si tu alifunga bao la kusawazisha katika dakika za majeruhi, lakini dakika mbili baadaye akatoa asisti kwa kocha wa sasa wa mashetani 'Mashetani Wekundu' hao, Ole Gunnar Solskjaer aliyefunga bao la ushindi. Aliingia kwenye kumbukumbu ya aina yake, licha ya siku hiyo kuwa na umri wa miaka 33. Pamoja na yote alifikisha asisti 76 na kufunga mabao 146 kwa kipindi chake cha uchezaji.

### 2. DENNIS BERGKAMP – ASISTI 94

Huyu ni gwiji wa Uholanzi ambaye alikuwa kwenye kikosi cha Arsenal kilichokuwa bora zaidi chini ya kocha, Arsene Wenger.

Alianza kucheza kama kiungo na baadaye akawa mshambuliaji wa pili yaani namba 10. Yeye mara zote alikuwa mpishi wa mabao zaidi kuliko kufunga. Kwa kipindi chake alitengeneza asisti 94 kwa jina lake na kubaki kuwa mmoja wa alama ya Arsenal.


### 1. WAYNE ROONEY – ASISTI 103

Wayne Rooney Muingereza huyu ndiye anayeshikilia rekodi ya asisti nyingi hadi sasa kwenye Ligi Kuu ya England.

Amecheza kwa misimu 16 kwenye Ligi Kuu ya England akianzia klabu yake ya utotoni, Everton kabla ya kuwa na mafanikio makubwa pale Manchester United na sasa anamalizia soka kule Derby County.

## ISIKUPITE

ERLING Braut Haaland amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga bao kwenye Bundesliga baada ya ligi hiyo kurejea Jumamosi kutokana na kusimama kwa kipindi kirefu kwa sababu ya mlipuko wa virusi vya corona [COVID-19]. Haaland alifunga bao hilo dakika ya 24 wakati Borussia Dortmund ikishinda 4-0 dhidi ya Schalke. Mabao mengine yalifungwa na Raphael Guerreiro (dk. 45' na 63') pamoja na Thorgen Hazard dakika ya 48.



Extra Time

# MAKOCHA WA5 BORA WASIO NA KAZI NA KLABU ZINAZOWAFAA

**LONDON,** England

KUWA kocha ni moja ya kazi ngumu katika soka. Kuwasimamia wachezaji wenye tabia tofauti na kujaribu kuhakikisha unapata kilichobora kutoka kwao mara zote si kazi rahisi. Ongeza hilo na presha kutoka kwa wamiliki wa klabu, pamoja vyombo vya habari visivyosamehe, kwa hakika ni kazi ngumu.

**Kocha anahitaji kuipa klabu utambulisho. Wakati tunapofikiria kuhusu Pep Guardiola, tunafikiria kuhusu staili ya soka la tiki-taka. Jurgen Kloop anajulikana kwa staili ya soka la kusukumiza mashabulizi mbele, na Sir Alex Ferguson anatukumbusha soka la kushambulia kwa haraka na mashambulizi ya kushitukiza.**

Zamani, alitakiwa kufanya kila kitu, kuanzia kufanya skauti ya wachezaji, usajili na udhamini. Yaani klabu ilikuwa inaendeshwa na kocha. Leo hii kazi ya kocha mkuu inahusika tu kwa kile kinachotokea uwanjani.

Hapa tunawaangalia makocha bora watano ambao kwa sasa hawana kazi na klabu bora zinazowafaa, twende sasa...

### #5. LAURENT BLANC

Umekuwa ni muda mrefu sasa tangu Laurent Blanc alipokuwa kocha wa Klabu. Mara ya mwisho alionekana kama kocha wa PSG, na kuwaongoza kwenye mataji matatu mfululizo ya Ligi Kuu, Blanc ni gwiji wa soka la Ufaransa, kwa pamoja kama mchezaji na kocha.

Wakati muda mwingi alikuwa PSG, awali pia aliwahi kuinoa Bourdeaux. Aliongoza timu yake kutwaa mataji matatu mwaka 2008, na akapewa kazi ya kuinoa timu ya Taifa ya Ufaransa. Msimu wake wa mwisho haukuwa mzuri kwa mujibu wa rais wa klabu, alishindwa kufuzu robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Na tangu hapo hakuna kocha yeyote aliyeiwezesha PSG kusonga mbele ya hatua hiyo katika mashindano hayo.

Yeye ni aina ya kocha ambaye anaweza kuja kwenye kikosi ambacho kipo tayari kushindana kwenye mashindano makubwa, lakini bado hajakuwa hapo.

### KLABU INAYOMFAA: OLYMPIQUE LYON

Wakati Lyon inawachezaji nyota wa kuinyanyua kama Memphis Depay, Moussa Dembele na Houssem Aouar, bado wamemaliza nafasi ya saba, na wanataka mtu atakayeweza kuwarudisha kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Blanc, kwa ujuzi wake na kulielewa soka la Ufaransa, ni mtu anayewafaa.

### #4. MARCELINHO

Marcelinho ni mmoja wa makocha wachache duniani ambaye anaweza zaidi kuutumia mfumo wa 4-4-2 na kupata mafanikio. Alikuwa kwenye kiwango cha juu wakati wake pale Villareal ambapo aliwachukua kutoka ligi daraja la pili hadi kwenye nusu fainali ya Ligi ya Europa.

Pia ana jicho la kuona vipaji.Aliwauza wachezaji kama Bailly, Vietto, na Pato kwa kiasi kikubwa cha fedha.

Ni kocha mwenye ujuzi, anajua namna ya kuwapata wachezaji. Msimu wake wa mwisho na Valencia, alishinda Kombe la Mfalme ['Copa del Rey'], akiifunga Barcelona kwenye fainali. Kwa mshangao, alifukuzwa baada ya mechi tatu tu msimu huu.

Uwezo wake wa kufanya kazi kwa bajeti ndogo unamfanya kuwa na uwezo mzuri wa kufundisha klabu zilizopo katikati ya msimu kuanzia 5-bora.

### KLABU INAYOMFAA: WEST HAM

West Ham tayari wana kikosi kizuri kwenye karatasi. Haller, Anderson, Diop na Fornals- wote wapo tayari kusukumwa, angalau kwenye Ligi ya Europa. Pamoja na heshima zote kwa David Moyes, yeye si mtu anayeweza kufanya hivyo. Marcelinho anaweza kuwa mtu atakayeisaidia klabu hiyo kufika sehemu inayotakiwa kuwapo.

### #3. UNAI EMERY

Kabla ya kukutana na wakati mgumu pale Arsenal, Unai Emery alikuwa na CV nzuri. Mataji matatu mfululizo kwenye Ligi ya Europa akiwa na Sevilla na mataji saba akiwa pale PSG yalitosha kuwashawishi 'Washikabunduki' kwamba alikuwa mtu sahihi kuwaongoza.

Soka la kushambulia kwa kasi ndio kitu kilichotengeneza jina la Emery. Hata pale Arsenal, kulikuwa na ishara ya hilo, lakini kutokana na safu mbovu ya ulinzi kazi ikawa ngumu kwake. Klabu ambayo ipo tayari kuamini uwezo wake itakuwa sahihi kwake.

### KLABU INAYOMFAA: NAPOLI

Napoli imekuwa na msimu mbaya, huku Rais wa Klabu, Aurelio de Laurentiis akiwa ameonyesha hadharani kutoelewana na wachezaji. Wachezaji wengi muhimu kama Koulibaly na Allan wanatarajia kuuzwa kipindi cha majira ya joto kinachokuja. Wana kocha mzuri Gattuso, lakini Napoli inahitaji kocha wa daraja la juu mwenye uwezo wa kuleta ushindani kwenye Serie A kwa mara nyingine tena.

Emery anaweza kuwa kocha atakayefiti kwa klabu hiyo. Kama wakifanya usajili sahihi kuziba mapengo ya wachezaji wanaoondoka, Napoli inaweza kuwa kama Juventus, Inter Milan na Lazio endapo watatumia fedha zao.

### #2. MASSIMILIANO ALLEGRI

Kwa kila kitu Max Allegri amefanikiwa, hapati heshima inayotakiwa. Huku akiwa na mataji sita ya Serie A, ya ligi manne na matatu ya Italian Supercups, pamoja na fainali mbili za Ligi ya Mabingwa Ulaya, inatosha kusema ni kocha mwenye mafanikio sana.

Huku ikiwa inakaribia miezi 18 tangu awe hana klabu ya kuinoa, atakuwa tayari kupata kazi haraka. Timu ya Allegri inakuwa imejengwa na safu imara ya ulinzi. Wakati akiwa kocha wa Juventus, waliruhusu mabao 25 kwenye ligi kwa msimu.

Wakati wake pia amewanoa wachezaji bora kama Buffon, Barzagli, Evra, Pirlo, Tevez na Dani Alves.

### KLABU INAYOMFAA: ATLETICO MADRID

Inaweza kuonekana ni kitu kigumu kutokana na kile ambacho Diego Simeone amefanikiwa pale Atletico Madrid, lakini pengine inaweza kuwa ameshafikia kilele chake cha mafanikio. Ni wakati wake sasa kuachia nafasi hiyo kwa mtu mwingine.

Ishara zinaonekana, kwa sasa wapo nafasi ya sita kwenye LaLiga, na wameiondoa Liverpool kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Walipofika sasa, Simeone anatakiwa kuachia na Allegri anaweza kufiti kwenye kiti hicho.

### #1. MAURICIO POCHETTINO

Kuchomoza kwa Mauricio Pochettino katika soka la dunia hii ni kutokana na jitihada zake mwenyewe. Kuchomoza kwa Tottenham Hotspur kuwa moja ya vigogo kwenye Ligi Kuu ya England, ni kazi yake. Kwa kile alichofanikiwa Pochettino kwa klabu ambayo inachukuliwa kama haina vyanzo vingi vya fedha, kumemfanya kuwa na jina kubwa duniani.

Ingawa hajawahi kushinda taji lolote na klabu hiyo, ameichukua klabu hiyo kutoka katikati ya msimamo hadi kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Inakaribia miezi sita sasa tangu alipofukuzwa, na amekuwa akihusishwa na klabu nyingi duniani. Barcelona, Real Madrid, PSG na Newcastle, zote amekuwa akihusishwa nazo.

Tangu kuwapo na taarifa za Newcastle kununuliwa na matajiri wa Saudi Arabia, amekuwa akitajwa sana kama ndiye anayekwenda kuchukua mikoba ya kuinoa.

### KLABU INAYOMFAA: MANCHESTER UNITED

Huku Pochettino akiwa anachukuliwa kama mmoja wa makocha watatu wa daraja la juu duniani, anafaa kuwa kwenye moja ya klabu bora. Ingawa Ole Gunnar Solskjaer amesaini mkataba mpya, United haijawa na matokeo ya kuridhisha tangu raia huyo wa Norway achukue kazi hiyo.

Pochettino ni aina ya mtu ambaye United inamhitaji ili kuirudisha kuwa klabu yenye kushinda katika kila mashindano. Tayari wana kikosi kizuri, na usajili wa wachezaji wengine utakuwa unahitajika. Pochettino anaweza kuwa mtu sahihi wa kufiti kwenye viatu vya Sir Alex Ferguson.



POCHETTINO

## Nukuu

"Sijawa na mawasiliano yoyote ya uwanjani na Messi, nimezungumza naye kwa njia ya simu mara nyingi. Sijamuona akijifua mazoezini, nimepishana naye tu kwenye sehemu ya kupaki magari mara nyingi. Wachezaji wote wanafanya mazoezi katika viwanja tofauti, mimi nipo na Sergi Roberto na (Sergio) kwenye uwanja mmoja, lakini tumetengwa," **Beki wa Barcelona, Gerard Pique**



"Unakwenda kule wanakotaka, kwa sasa naishi Valencia ili kuwa na mwanangu, ila nimejiandikisha jijini Madrid. Lakini sijui kituo changu cha kwanza kitakachofuata kitakuwa wapi, nipo wazi kwa kila kitu. Kitu kilichopo wazi ni kwamba, Atletico wana [Diego] Simeone ambaye anaweza kuwa nao hadi pale yeye mwenyewe atakapoamua kuondoka. Kwa sababu hakuna anayefiti pale zaidi ya yeye," **Kocha wa zamani wa Arsenal, Unai Emery**



"Ninamchagua Virgil van Dijk, inashangaza, kwa sababu hajakuwa kwenye mchezo huo kwa muda mrefu, hasa ikizingatiwa kwamba kuna majina makubwa kama– John Terry na Rio Ferdinand, watu ambao wamecheza kwa muda mrefu. Lakini ishara zimeonyesha katika miaka yake michache, na kwamba angekuwa kwa muda mrefu angekuwa daraja la juu kabisa," **Beki wa zamani wa Manchester City, Vincent Kompany, akimuelezea Van Dijk kama beki bora wa kati Ligi Kuu England**





# WABURUZA MKIA WATANO LIGI BARA NA TUMBO JOTO

Kikosi cha Singida United kinachoshika mkia kwenye Ligi Kuu Bara. **PICHA: MAKTABA**

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya Serikali kutangaza inatarajia kuruhusu Ligi Kuu Bara kurejea, jambo litakalofanikisha bingwa wa ligi hiyo kupatikana uwanjani, na pia timu zitakazopanda kutoka Ligi Daraja la Kwanza pamoja na zile zitakazoshuka daraja, tayari viongozi wa timu zilizopo chini ya msimamo wa Ligi Kuu, matumbo yao yameonekana kuwa na joto la hofu.

**Baada ya janga la ugonjwa wa COVID-19 unaosababishwa na vizuri vya corona, kulizuka maoni mengi, huku baadhi wakitaka Ligi Kuu ifutwe kama vile ilivyofanywa kwenye baadhi ya nchi duniani.**

Baadhi ya nchi duniani zimefuta ligi zao na kutoa ubingwa kwa timu zilizopo juu, huku zikiziacha timu za chini kwenye msimamo zikiendelea kupeta.

Ina maana hakuna timu zilizoshuka. Ukisikiliza maoni ya viongozi wengi hasa zilizokuwa chini ya msimamo walikuwa wakitaka Simba apewe ubingwa, lakini huku chini ya msimamo kusiwe na timu itakayoshuka daraja msimu huu.

Hata hivyo, urejeo wa Ligi Kuu kama kusudio la serikali, zimewaacha tumbo joto timu ambazo tayari zilishaanza kuona huenda zingebakishwa na kuiacha Gwambina FC ambayo inatakiwa kushinda mechi mbili tu kati ya nne ilizonazo kusubiri msimu ujao kupanda Ligi Kuu.

Kwenye makala haya, tunawaletea timu ambazo ziko kwenye hatari ya kushuka daraja, na sasa zinatakiwa zijiandae kisawasawa ili zitumie nguvu zao za uwanjani kutoshuka daraja, na si mteremko...

**1. SINGIDA UNITED (POINTI 15)**

Singida United ndiyo timu yenye hatari zaidi ya kushuka daraja kwenye Ligi Kuu kuliko timu nyingine yoyote ile. Wapo wachambuzi wanaona ni kama tayari imeshuka kiuhasilia, lakini si kimahesabu. Ina pointi 15 tu mpaka sasa ikiwa imesaliwa na mechi tisa tu.

Si tu kwamba inashika mkia ikiwa chini, lakini inazidiwa pointi nane na timu iliyokuwa juu yake, Mbao FC. Mpaka ligi inasimamishwa, mechi ya mwisho iliifunga Mbeya City mabao 2-1, ikitoka kupoteza mechi nne mfululizo.

**2. MBAO FC (POINTI 23)**

Ni timu ambayo imeshangaza wengi msimu huu kutokuwa na kiwango cha kawaida, kilichozoeleka. Inaweza kabisa ikawa ndiyo msimu wao wa mwisho kucheza Ligi Kuu, tangu ilipopandishwa na Shirikisho la Soka nchini (TFF) msimu wa 2016/17 kutokana na tuhuma za upangaji matokeo kwa timu za Geita Gold, JKT Kanembwa, Polisi Tabora na JKT Oljoro.

Iliingia kwenye Ligi Kuu na kuwa timu ya kutisha. Lakini kila msimu inaonekana kupungua makali, huku msimu huu ikiwa kwenye hatari zaidi kuliko wakati mwingine wowote. Ina pointi 23, ikibakiza mechi tisa tu, ikishika nafasi ya 19.

**3. ALLIANCE FC (POINTI 29)**

Ina pointi 29 ambazo bado haziwezi kuiweka salama kubaki Ligi Kuu msimu huu, bali inabidi ijifunge kibwebwe kisawasawa. Kinachotoa shaka zaidi ni kwamba Alliance ndiyo timu iliyopoteza mechi zote tano za mwisho mfululizo, hadi pale ligi ilipositsimama kutokana na ugonjwa wa COVID-19. Inakamata nafasi ya 18, hivyo nayo imo ndani ya zile timu nne zinazonukia kushuka daraja. Ni ushindi mfululizo unaohitajika katika mechi tisa ilizobakisha kwenye ligi ili ijikwamue.

**4. MBEYA CITY (POINTI 30)**

Cha kusikitisha msimu huu ni kwamba zile timu ambazo miaka michache tu iliyopita zilitamba, ziko hoi bin-taaban. Nazizungumzia Singida United, Mbao FC na hii ni Mbeya City.

Ilileta mapinduzi makubwa msimu wa 2013/14, kiasi kwamba kila timu iliyokuwa ikitaka kupanda ilitaka kuwa kama Mbeya City. Kwa sasa iko taaban, ikiwa moja kati ya timu zinazohesabiwa kuwa zitashuka msimu huu kama zikikaa vibaya. Inakamata nafasi ya 17, ikiwa na pointi 30. Iwapo haitojirekebisha kwenye mechi zake tisa zilizobaki, msimu ujao inaweza isiwapo Ligi Kuu.


**5. NDANDA FC (POINTI 31)**

Hii ndiyo timu yenye bahati kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, kwani misimu yote iliyokuwa kwenye ligi imekuwa ikipona kushuka dakika za mwisho. Wengi wanataka kuona kama msimu huu nao wanaweza kupona tena. Ni timu ambayo miaka yote ina 'zali' la kubaki kwenye zile mechi za mwisho. Msimu huu kama kawaida, inashika nafasi ya 16, ikiwa na pointi 31. Kwa mechi za karibuni kabla ya kusimamishwa, ilikuwa imeanza kufanya vema kama kawaida yake. Hata hivyo, waswahili wanasema 'siyo kila siku ni Ijumaa'. Mechi zake tisa zilizobaki zitatoa jibu.

**JE, WAJUA?**



SERGIO Ramos ndiye mchezaji aliyecheza mechi nyingi zaidi timu ya Taifa ya Hispania akiwa ameichezea mara 170, aliweka rekodi hiyo Oktoba, mwaka jana, kwa kumpiku nyota wa zamani wa Real Madrid, kipa Iker Casillas, aliyekuwa ameichezea mara 168.





# Corona yapaisha bei ya tende

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa ugonjwa wa corona umesababisha bei ya tende kupanda, huku zikiadimika katika maeneo mengi ulimwenguni hususan kipindi cha mfungo wa Ramadhani.

Kufuatia hali hiyo, Taasisi ya Misaada ya Miraji Tanzania, imetoa msaada wa tani moja ya tende, kwa waumini wa dini ya kiislamu wasiojiweza ikiwamo wajane wa Mkoa wa Dodoma ili kukidhi mahitaji yao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mwenyekiti wa Taasisi hiyo mkoani humo, Athumani Hotty, alisema wameamua kugawa msaada huo kutokana na umuhimu wa tende katika mfungo huo.

Alisema kutokana na kuwa adimu, lakini pia zinapatikana kwa bei ya juu hali inayowawia vigumu watu wasiojiweza kununua.

"Sisi tumeona ipo haja ya kutoa msaada huu kwa makundi haya maalum, tende kwa waumini wa dini ya kiislamu tunaelekezwa kuwa kabla ya kufungua Muislamu anatakiwa afungue kwa kula tende kutoka na kuwa inavirutubisho vingi ambavyo vinamsadia mtu aliyefunga kwa siku nzima," alisema Hotty.

Aidha, aliwataka waumini hao katika mfungo huo kuendelea kuzingatia maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya katika kujikinga na virusi vya corona.

"Katika maeneo yetu ya misikiti tunasisitiza waumini kuendelea kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya kwa kunawa mikono, kuvaa barakoa, lakini pia kutoshiriki katika mikusanyiko ambayo ni eneo hatari kwa virusi hivi vya corona," alisema Hotty.

Pia alisema kupitia Baraza kuu la Waislamu Tanzania (Bakwata) mkoa wa Dodoma, wamekuwa wakitoa semina kwa maimamu wa misikiti yote namna ya kujikinga na ugonjwa huo katika nyumba zao za ibada.

Vilevile, alisema pamoja na kutoa semina kwa Maimamu hao, pia wanatoa misaada ya vifaa vya kujikinga na maambukizo ya corona kwenye maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

# Wachungaji Anglikana wapewa vifaa corona

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KANISA la Anglikana Dayosisi ya Dodoma, limetoa vifaa vya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona kwa wachungaji na watu mbalimbali jijini Dodoma vyenye thamani ya Sh. milioni 61.

Akizungumza katika utoaji vifaa hivyo sambamba na semina ya kujikinga na maambuzo ya virusi vya corona kwa viongozi wa dini, Askofu wa Dayosisi hiyo, Dickson Chilongani, alisema wachungaji ni kundi ambalo lipo katika hatari ya kupata ugonjwa huo kwa sababu wanakutana na waumini wengi wakati wa ibada wanazoendesha.

Dk. Chilongani alisema wameamua watoe mafunzo kwa watumishi hao namna ya kujikinga ili wanaporudi kwenye parishi zao waelimishe waumini jinsi ya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa huo.

Akifungua mafunzo hayo, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, aliishukuru Dayosisi hiyo kwa kuonyesha jitihada za kuiunga mkono serikali katika jitihada za kupambana na corona.

Katambi alisema semina hiyo imetolewa kwa watu muhimu ambao wanakutana na waumini kila mara.

"Mmefanya vizuri kufundisha hii semina kwa sababu watumishi watasaidia kuwafundisha waumini namna ya kujikinga na ugonjwa huu," alisema.

Alisisitiza wananchi kuendelea kujikinga na kuchukua tahadhari kwa sababu ugonjwa bado upo kwa jamii.

Aliwataka kufuata masharti ya wataalamu wa afya yanayotolewa ya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa huo.



Katibu wa Jumuiya ya Wanawake ya Chama Cha Mapinduzi Tanzania (UWT) Wilaya ya Dodoma, Diana Madukwa (kushoto), akimkabidhi Rhoda Andrea, ambaye ni mgonjwa wa ukoma , vifaa vya kunawa mikono kwa ajili ya kujikinga na corona, viongozi wa jumuiya hiyo walitembelea kambi ya wagonjwa wa ukoma ya Msamaria Mwema Homolo jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yaombwa umeme kituo cha Msamaria Hombolo

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA.

WALEMAVU wa ugonjwa wa ukoma wanaoishi kwenye Kituo cha Msamaria Mwema Hombolo jijini Dodoma, wameomba serikali kuwasaidia umeme ili waanzishe miradi itakayowasaidia kukidhi mahitaji yao.

Ombi hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na walemavu hao mara baada ya kupokea vifaa vya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa corona na vyakula kutoka Jumuiya ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Wilaya ya Dodoma walipotembelea kituo hicho.

Mmoja wa wazee ambaye ana ulemavu uliotokana na ugonjwa huo, Simon Madanya, alisema kituo hicho hakina umeme, wamekuwa wakiishi kwenye mazingira ya giza na kuibiwa vitu wanavyosaidiwa na watu mbalimbali.

Alisema baadhi ya watu wasio waadilifu wamekuwa wakiingia na kuwaibia vitu walivyopewa msaada na wasamaria wema kwenye kituo hicho.

Aidha, Mdanya alisema uwapo wa umeme utawasaidia walemavu hao kuutumia kuanzisha miradi midogo ya kiuchumi kama ushonaji kwa kutumia cherehani za umeme na kufungua biashara ya kuuza mabarafu kwa wavuvi waliopo bwawa la Hombolo.

"Tunawashukuru sana UWT kwa kutukumbuka, lakini tunaomba kusaidiwa tatizo la umeme kwa sababu imekuwa kero kwetu na sisi hatuna fedha za kuunganisha umeme," alisema.

Naye Mwenyekiti wa watu wenye ulemavu wa kituo hicho, Michael Mtonyi, alisema kituo hicho kina kaya 29 zenye watu 250, ikiwamo watu wenye walemavu 35.

Mtonyi alisema kituo hicho kilianzishwa mwaka 1997 ikiwa ni msaada kutoka Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Central Tanganyika (DCT) kwa ajili ya kutunza walemavu wa ugonjwa wa ukoma walikuwa wakiomba omba mitaani.

Akizungumza baada ya kukabidhi msaada huo, Katibu wa UWT wilayani humo, Diana Madukwa, alisema wameona ni muhimu kukabidhi msaada huo ili kuunga mkono juhudi za serikali za kupambana na Corona.

Madukwa alisema wamekabidhi vifaa mbalimbali na vyakula vyenye thamani ya Sh. milioni moja na kuwataka viongozi wa eneo hilo kuhakikisha vinawafikia walengwa wote.

"Nimesikia kuna malalamiko ya wazee hawa kudai kunyimwa baadhi ya misaada inayoletwa na wasamaria wema ,ninawaagiza viongozi wa kituo na Mwenyekiti wa Mtaa huu kuhakikisha msaada huu unawafikia walengwa ,nitafanya ziara yangu kimya kimya nikisikia hilo tena tutawachulia hatua," alisema.

HABARI MBEYA

# Serikali yakiri kutokuandaa Kanzi data ya wajasiriamali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKOA wa Mbeya umekiri kuwa haukuandaa kanzi data ya wafanyabiashara wadogo waliopatiwa vitambulisho vya ujasiriamali vilivyotolewa na Rais John Magufuli mwaka jana, hivyo kushindwa kufanya tathmini ya ukuaji wa wafanyabiashara hao.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Mkoa huo, Albert Chalamila, alipokuwa anakabidhiwa vitambulisho vipya 15,000 na Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wa Mkoa huo, Eunice Mhaluka.

Alisema hali hiyo imesababisha kushindwa kuwabaini wajasiriamali ambao wamekuwa kiuchumi na hawastahili kuendelea kupewa vitambulisho hivyo na badala yake wanatakiwa waingie kwenye mfumo rasmi wa ulipaji kodi unaosimamiwa na TRA.

"Tumeletewa vitambulisho vipya ambavyo tunatakiwa kuviuza kwa wajasiriamali, sasa nawaagiza maofisa biashara wa Halmashauri zote kuandaa kanzi data ya wajasiriamali hawa ili kuwa na utaratibu mzuri wa kufuatilia ukuaji wake," alisema Chalamila.

Aidha aliwataka wakuu wa wilaya zote kutumia vyombo vyao kuwafuatilia wananchi wote watakaopatiwa vitambulisho, hivyo ili kuwabaini wasiostahili na kuwaondoa kwenye mfumo huo ambao unatoa msamaha wa kodi. Chalamila aliwataka wakuu wa wilaya kuendelea kuwaelimisha wajasiriamali kuhusu kodi ambazo wamesamehewa kwa mujibu wa vitambulisho hivyo kwa maelezo kuwa baadhi yao wamekuwa wakiutumia msamaha huo vibaya.

Alisema baadhi wamekuwa wakigoma kulipa kodi za nyumba, gharama za kuondoa taka na michango mingine ambayo wanakubaliana katika maeneo yao kitu ambacho alisema sio sahihi.

Akitoa maelezo kuhusu vitambulisho hivyo, Meneja wa TRA Mkoa wa Mbeya, Eunice Mhaluka, alisema mwaka jana mkoa huo ulipatiwa vitambulisho 100,000 lakini mwaka huu vimepunguzwa na kuwa 86,000 ambavyo vitaendelea kuletwa kwa awamu.

Alisema katika awamu ya kwanza walipokea vitambulisho 15,000 ambavyo ndivyo walivyokabidhi, na kwamba wakipokea vingine wataendelea kuvigawa katika Halmashauri zote za Mkoa huo.

Alisisitiza kuwa watahakikisha wanavigawa kwa wajasiriamali wenye sifa pekee ambao ni wenye mauzo ghafi yasiyozidi Sh. 4,000,000, huku akisema kuwa baadhi ya wananchi katika awamu ya kwanza walikuwa wanatafsiri vibaya.

"Vitambulisho hivi vya awamu hii viko tofauti kidogo na vile vya mwaka jana, hivi vya sasa vina namba maalum na haviwezekani kughushi, tunaomba tushirikiane wote kutoa elimu kwa wajasiriamali wetu," alisema Mhaluka.

Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Mbeya wa Uchumi na uzalishaji, Said Madito, alisema ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza mwaka jana kwenye vitambulisho hivyo, serikali imetoa utaratibu maalum wa kukabidhi.

Alisema Meneja wa TRA anamsainisha Mkuu wa Mkoa nyaraka maalumu baada ya kumkabidhi na kisha Mkuu wa Mkoa anavikabidhi kwa wakuu wa wilaya.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (kushoto), akipokea moja ya makasha yenye vitambulisho vya wajasiriamali 15,000, ambavyo vimetolewa na Rais John Magufuli kutoka kwa Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Mbeya, Eunice. Makabidhiano hayo yalifanyika mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Abiria wa mabasi wasiovaa barakoa watangaziwa kiama

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KAMATI ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Mbeya ikiongozwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, William Ntinika, imeanza kufanya operesheni maalumu ya kukagua na kuwachukulia hatua abiria wote wa magari ya abiria ambao hawavai barakoa.

Mkuu huyo wa wilaya alisema kwamba lengo la hatua hiyo ni kukabiliana na maambukizo ya virusi vya corona.

Operesheni hiyo ilianza mwishoni mwa wiki ambapo wajumbe wa Kamati hiyo walikuwa wanazunguka katika vituo mbalimbali vya magari ya abiria daladala) na kwenye baadhi ya barabara na kukagua ili kuona kama abiria wanavaa barakoa.

Ntinika alisema kutokana na tishio la ugonjwa huo umewekwa utaratibu wa kulazimisha kila abiria wa daladala na bajaji mkoani humo kuvaa barakoa na kwamba kwa wale ambao wanakaidi watakuwa wanashushwa kwenye magari na kuchukuliwa hatua.

Alisema elimu imetolewa vya kutosha na wataalamu lakini baadhi ya watu wamekuwa wakikaidi maelekezo yanayotolewa hali ambayo inaweza kusababisha ongezeko la maambukizo ya corona.

"Tumeamua tuanze kukagua kwenye magari ili kuhakikisha wananchi wetu wanavaa barakoa, ukivaa barakoa unajikinga mwenyewe na ugonjwa huo, lakini pia kama una maambukizo unawakinga wenzio," alisema Ntinika.

Alisema Serikali imewarahisishia wananchi kwa kuruhusu hata barakoa za vitambaa zitumike ambazo gharama yake ni nafuu na hivyo hakuna sababu ya watu kutozinunua na kuvaa.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema zoezi hilo litakuwa endelevu mpaka pale ambapo wananchi wote wataanza kufuata maelekezo hayo.

Alisema wakati wa operesheni hiyo walibaini kuwa mwitikio umekuwa mzuri kwa baadhi ya wananchi isipokuwa wachache ambao alisema wataendelea kuwashughulikia wakiwabaini.

"Wengi wanajitahidi kufuata maelekezo maana wamejitahidi kuvaa barakoa, lakini tutaendelea kufuatilia na kuwachukulia hatua wote wanaokiuka utaratibu huu," alisema Kamanda Matei.

Alisisitiza kuwa mbali na operesheni hiyo pia askari wa Kikosi cha Usalama barabarani, wanaendelea kufanya ukaguzi kwenye magari na kuchukua hatua ikiwamo kuwashusha abira ambao hawavai barakoa hizo.

Baadhi ya madereva na makondakta wa daladala waliishukuru Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa kuanzisha operesheni hiyo wakidai kuwa baadhi ya abiria wamekuwa wakikaidi wanapowapatia maelekezo ya kuvaa barakoa hizo.

# Wafanyabiashara washitukiwa ujanja kodi kisa corona

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wafanyabiashara mkoani Mbeya, wanadaiwa kuanza kukwepa kutoa risiti kwa wateja wao wanapowauzia bidhaa kwa kisingizio cha kuepuka kuambukizana virusi vya corona.

Hali hiyo inatafsiriwa kuwa ni ukwepaji wa kulipa kodi mbalimbali za serikali.

Baadhi ya wananchi wanadai kuwa tangu ugonjwa huo ulipotangazwa kuingia nchini, baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wakigoma kutoa risiti na hivyo kuwalazimisha na wao wawe sehemu ya wakwepa kodi.

Mmoja wa wananchi hao, Bruno John, Mkazi wa Uyole jijini Mbeya, alisema Serikali imekuwa ikisisitiza kuwa kila mwananchi anatakiwa kudai risiti anaponunua kitu chochote, lakini katika kipindi hiki hawapewi risiti hizo.

"Ukiwauliza wanasema serikali imezuia utoaji wa risiti kwa sababu ya ugonjwa huo, lakini tukiwauliza viongozi wa Serikali wanasema maelezo hayo siyo ya kweli, sasa tunashindwa kuelewa wanapata wapi ujasiri wa kuisingizia Serikali," alisema Bruno.

Naye Isack Mwaigaga, mkazi wa Iyunga jijini Mbeya aliiomba Serikali kutoa elimu upya kwa wananchi juu ya jambo hilo kwa maelezo kuwa mapato yanapotea kutokana na wafanyabiashara hao kutotoa risiti.

Alisema alienda katika Soko la Mwanjelwa kwa ajili ya kununua baadhi ya vitu lakini kila alipodai risiti ya kielektroniki (EFD) aliambiwa kuwa utaratibu wa utoaji wa risiti hizo umesitishwa.

Akizungumzia suala hilo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema ameshapokea malalamiko hayo na kwamba tayari ufuatiliaji wa siri unaendelea kufanyika katika maeneo mbalimbali ili kubaini ukweli wake.

Aliwataka wafanyabiashara mkoani humo kuendelea kufuata utaratibu kwa maelezo kuwa wao wanatumika na Serikali kama mawakala wa kukusanya mapato na hivyo akasisitiza kuwa watakaoendelea kukwepa watachukuliwa hatua kali za kisheria.

"Rais alishatoa maelekezo kwamba shughuli za uzalishaji mali ziendelee kama kawaida, sasa hawa wanaogoma kutoa risiti wanakiuka sheria, vyombo vyetu vipo kazini vinaendelea kufuatilia jambo hili na muda sio mrefu tutaanza kuchukua hatua," alisema Chalamila.

Aliwataka wananchi mkoani humo kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kujiletea maendeleo, na kwamba wapotoshaji wa taarifa za corona wataendelea kuchukuliwa hatua za kisheria.

# W/biashara wazalendo wamkuna Balozi Iddi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema mchango mkubwa wanaoendelea kutolewa na wafanyabiashara wazalendo nchini utabakia kuwa ukumbusho kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Balozi Seif Ali Iddi alisema hayo jana, wakati akipokea msaada wa vifaa mbali mbali kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum ofisini kwake Vuga mjini Zanzibar vilivyotolewa na Mwenyekiti wa kampuni za ZAT na Royal Group, Mohamed Raza Hassanali.

Raza ambae pia ni Mwakilishi wa Jimbo la Uzini, alikabidhi barakoa 400 kwa wananchi wa jimbo hilo pamoja na vyakula kwa ajili ya familia 218 zilizokumbwa na maafa kutokana na mvua zilizonyesha hivi karibuni.

Balozi Iddi alisema wananchi wengi wanafarijika kutokana uamuzi wa wafanyabiashara wazalendo wanaounga mkono matatizo na majanga yanayowakumba katika maeneo yao.

Aidha, alipongeza kampuni hizo kwa jitihada zinazochukuliwa kuwa karibu na wananchi sambamba na Serikali katika kuona ustawi wa Jamii unaendelea kubakia salama na furaha licha ya changamoto zinazojitokeza.

Akizungumzia athari ya mafuriko ya mvua za masika za mwaka huu, Balozi Iddi ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar, aliwatahadhari wananchi kuendelea kuepuka kujenga makazi yao ya kudumu katika maeneo hatarishi.

Alisema maeneo ya kilimo, sehemu za mabwawa, mito pamoja na misingi ya maji ya mvua ni vyema zikaepukwa mapema ili kujihakikishia usalama wa maisha yao sambamba na hasara kubwa inayoweza kuleta usumbufu wa mchanganyiko wa mawazo yasiyokwisha ndani ya maisha yao.

Naye, Mohamed Raza Hassanali, alisema uongozi wa taasisi hizo umefikia hatua ya kutoa msaada huo kufuatia changamoto mbali mbali zinazowakumba watu wenye mahitaji maalum.

Akitoa shukrani kwa niaba ya uongozi, watendaji wa idara ya watu wenye ulemavu pamoja na watu wenye mahitaji maalum, Ofisa Jinsia Maendeleo wa Idara hiyo, Foum Shaaban, alisema milango bado iko wazi kwa mtu au taasisi yoyote ndani na nje ya nchi kusaidia kundi hilo la watu wenye mahitaji maalum.

Foum alisema msaada huo wa baiskeli za walemavu, vyarahani pamoja na fimbo maalum za kuwaongoza watu wasioona zitagaiwa kwa wahusika Unguja na Pemba kwa mujibu wa taratibu zilivyopangwa.




Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Shaaban Seif Mohamed (kulia) akipokea Hundi ya Sh. 8,400,000/- kutoka kwa Uongozi na Wanachama wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Kuweka na Kukopa Zanzibar (ZASCU). **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Wawakilishi wataka msemaji wa Serikali

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wameitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuiga mfumo wa upande wa Muungano kuwapo kwa nafasi ya msemaji mkuu wa Serikali.

Baadhi ya majukumu yake ni kutoa ufafanuzi wa taarifa mbalimbali za upotoshaji za kuwakashifu viongozi na Serikali yake.

Mwakilishi wa jimbo la Shauri Moyo, Hamza Hassan Juma, alipongeza kazi kubwa inayofanywa na Msemaji Mkuu wa Serikali wa Serikali ya Muungano, Hassan Abbas, wa kutoa ufafanuzi na kujibu hoja kwa wakati ikiwamo za watu wasioitakia mema Serikali.

Hamza aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, na kusema kuwa anasikitishwa na kauli za kuikashifu Serikali ya Zanzibar zinazotolewa na baadhi ya watu ambao wanatoka katika familia maarufu Zanzibar huku hoja hizo zikishindwa kutolewa ufafanuzi wake.

Alisema ni jambo la ajabu sana kuona Serikali inakashifiwa na kutukanwa pamoja na CCM huku hakuna mtu anayejibu tuhuma hizo.

Alisema Msemaji wa Serikali, Hassan Abbas, anafanya kazi kubwa ya kujibu hoja na kutoa ufafanuzi pamoja na kueleza mambo mazuri yanayofanywa na Serikali huku pia akitoa maelezo ya kasoro ziliopo na juhudi zinazochukuliwa kwa sasa.

''Nachukuwa nafasi ya kumpongeza msemaji wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hassan Abasi, kwa kazi kubwa anayoifanya katika kufafanua mambo mbali mbali yanayohusu Serikali ambapo na sisi Zanzibar tunatakiwa kuiga utendaji wa aina hiyo,” alisema.

Hamza alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya mambo makubwa ikiwamo kutoa Elimu bure na kufuta michango ambayo ilikuwa ikitolewa na wazazi ikiwamo wale wenye uwezo mdogo wa kiuchumi.

Aidha, alisema huduma nyingi zinatolewa bure matibabu kwa wananchi wote ikiwemo vipimo vya wagonjwa huku Serikali ikitoa pencheni ya jamii kwa wazee waliofikisha umri wa miaka 70 bila ya kubaguwa.

# DC ataka wananchi kutunza kingo za mito

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MKUU wa Wilaya ya Magharibi ‘A’, Abeid Juma Ali, amewataka wananchi wanaokaa pembezoni ya mito na maeneo ya vyanzo vya maji kuacha kuchimba mchanga ili kuepukana na uharibifu wa mazingira.

Akizungumza katika ziara ya kuangalia uharibifu wa mazingira ya Mto Welezo uliotokana na uchimbaji wa mchanga, alisema eneo hilo linapaswa kuenziwa kwani lina vyanzo vingi vya maji na makazi ya watu.

Alieleza kuwa uchimbaji wa mchanga katika maeneo hayo umeathiri mazingira na makazi ya watu, jambo ambalo linalopaswa kuchukuliwa hatua za dharura na wadau wote. Aidha, aliwataka wananchi wa maeneo hayo kushirikiana na uongozi wa Shehia ya Welezo, idara ya misitu na rasilimali zisizorejesheka na manispaa ya Magharibi ‘A’ kuwadhibiti vijana wanaojihusisha na shughuli hizo ili kuepukana na madhara zaidi.

“Viongozi wa Shehia ninataka mwatambue na ikifika Jumatatu ijayo muwasilishe majina ya watu wanaochimba mchanga ili vyombo vinavyohusika vichukue hatua dhidi yao,” alielekeza Mkuu huyo wa wilaya.

Wakizungumza katika ziara hiyo, wananchi wanaoishi pembezoni mwa mto huo, walieleza kuwa mara kadhaa wamewasiliana na viongozi wa Shehia hiyo kuelezea changamoto wanayoipata pindi wanapokabiliana na watu wanaochimba mchanga ambao mara nyingi wamekuwa wakitumia vitisho.

“Kuna wakati huchimba usiku, lakini katika kipindi hiki cha mvua huchukua mchanga mtoni mchana na tunapowafuata hututishia maisha,” alieleza Omar Abdallah Mohammed.

Naye, Mkurugenzi wa Manispaa ya Magharibi ‘A’ , Amour Ali Mussa, alieleza kuwa watashirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kusimamia sheria ya uondoaji wanyama mijini ili kudhibiti magari ya ng’ombe na punda ambayo yanatumika katika uchimbaji wa mchanga.

“Huu ni ukiukwaji wa sheria, tunawaomba wananchi watupe taarifa kama walivyofanya leo ili tuchukue hatua zinazostahiki ikiwamo kutaifisha mchanga na vyombo vya usafiri vinavyotumika katika uchimbaji wa mchanga katika maeneo yote ya manispaa yetu,” alieleza Mkurugenzi huyo.

Zaidi ya tani 10 za mchanga zimepatikana zikiwa zimerundikwa kwa ajili ya kuuzwa katika eneo la Redio One shehia ya Welezo ambazo zimezuiliwa wakati uongozi wa wilaya hiyo ukiendelea na operesheni ya kuwabaini wamiliki wake kwa hatua zaidi.

# Sirro aombwa gari kituo cha polisi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANANCHI wa kata za Sabasabini na Bulungwa Halmshauri ya Ushetu, wilayani Kahama, wamemuomba Mkuu wa jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro (pichani), gari kwa ajili ya kituo kidogo cha polisi Bulungwa ili kudhibiti ujambazi na uvamizi wa maduka ya wafanyabiashara nyakati za usiku.



Maombi hayo waliyabainisha jana wakati wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti katika kata ya Bulungwa na sabasabini ambapo walisema kuwa, uvamizi na uporaji wa maduka ya wafanyabiashara wa kata hizo umekuwa ukifanyika wakati wa msimu wa mavuno.

Paschal Charles, Mwenyekiti wa serikali ya kijiji cha Sabasabini alisema kuwa gari lililopo katika kituo kidogo cha polisi Bulunga ni la tangu mwaka 1985 na nibovu, haliwezi kufanyakazi na limekuwa likisababisha polisi kuchelewa kufika kwenye eneo la tukio.

Alisema kuwa kituo cha polisi Bulungwa kimekuwa kikihudumia eneo kubwa ukilinganisha na vituo vingine vilivyopo Halmashauri ya Ushetu, maeneo hayo ni kata ya Mpunze, Sabasabini, Idahina, Igwamanoni, Ubagwe, Kinamapula pamoja na Nyankenda jirani na Msumbwe.

Nae Christina Paulo kutoka Bulungwa alisema kuwa, wamekuwa wakiwatuhumu Jeshi la Polisi vibaya na kukosa imani nao kutokana na kuchelewa kufika kwenye eneo la tukio na kukuta waharifu wameshaondoka na mali, huku waliojeruhiwa wameshapatiwa huduma ya kwanza.

"Tumekuwa tukivamiwa mara kwa mara kwenye maduka yetu ya biashara na makazi na kuporwa mali na wakati mwingine unavamiwa wakati umetoka kwenye mauzo ya Tumbaku, polisi wanachelewa kufika kwenye eneo la tukio kutokana na kukosekana kwa gari, alisema.

Akijibu malalamiko hayo, mmoja wa askari polisi aliyedai yeye sio msemaji wa polisi, alikiri kuwapo kwa changamoto ya kutokufika kwa wakati kwenye maeneo ya matukio kwa madai gari lililopo ni bovu na linazimazima wakati wakiwa kwenye doria.



Ofisa Usalama Mahali Pakazi wa kampuni ya Asas mkoani Iringa, Cosmas Charles (kushoto), akimkabidhi Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Mkoa, Dk. Alfred Mwakalebela, mashine ya kutakasa mwili jana kwa ajili ya kujikinga na virusi vya corona. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

## Mafia wapigwa msasa kuhusu ugonjwa corona

**Na Beatrice Philemon**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mafia, mkoani Pwani kupitia Idara ya Afya kwa kushirikiana na shirika la ActionAid Tanzania, wameanza kutoa mafunzo kwa wawezeshaji wa maendeleo katika ngazi ya jamii kuhusu ugonjwa wa COVID-19.

Lengo ni kuelimisha wananchi katika ngazi ya jamii kuhusu ugonjwa wa COVID-19, jinsi unavyoenea na jinsi ya kujikinga.

Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Zuberi Nzige, alisema kuwa wawezeshaji hao wametoka katika vijiji 23 vilivyopo katika wilaya ya Mafia ambao wanafanya kazi na shirika la ActionAid katika kuelimisha jamii kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia, ukiukwaji haki za wanawake, haki ya kumiliki ardhi na masuala mengine.

Alisema wameamua kutoa elimu hiyo baada ya kugundua kuwa asilimia kubwa ya wananchi wa Mafia bado hawajafahamu ugonjwa huu kwa sababu wananchi wengi hawana TV, Smartphone na pia hakuna redio za jamii ambazo zinaweza kuwasaidia kupata taarifa kuhusu ugonjwa huu au kuwaelimisha kuhusu ugonjwa huu.

Mafunzo hayo yalitolewa na Mganga Mkuu wa Wilaya kwa kushirikiana na Shirika la ActionAid Tanzania linalotekeleza mradi wa 'Local Rights Programme' katika Wilaya ya Mafia.

"Wakati wa mafunzo washiriki walifundishwa nini maana ya ugonjwa wa COVID-19, jinsi ya kutambua ugonjwa huu, jinsi unavyoambukizwa, dalili zake, jinsi ya kujikinga, jinsi ya kumgundua mtu mwenye ugonjwa wa corona na kutoa ushauri," alisema

Mbali na hilo pia walipewa namba ya simu ili mtu akigundulika katika vijiji vyao kuwa na ugonjwa huo waweze kutoa taarifa na mgonjwa aweze kuchukuliwa na kupewa huduma hospitalini

"Tumeamua kuwafundisha wawezeshaji hawa ili wawe mabalozi na pia kutusaidia kuelimisha jamii kuhusu ugonjwa huu katika ngazi ya jamii ikiwamo dalili zake, jinsi unavyoenea, jinsi ya kuzuia ugonjwa huu, jinsi ya kumgundua mtu mwenye COVID-19, na jinsi ya kujikinga ikiwamo kufuata taratibu zilizowekwa na serikali katika kujikinga na ugonjwa huu," alisema.

# Magufuli atekeleza ahadi kwa wakazi wa Masasi

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

HATIMAYE wakazi wa kata ya Nagaga Halmashauri ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, wameondokana na adha ya kubeba wagonjwa wao kwenye matenga,baiskeli na pikipiki baada ya Rais. John Magufuli kuwapatia msaada wa gari jipya la kubebea wagonjwa.

Gari hilo lina thamani ya Sh. Milioni 120 kwa ajili ya kutatua kero hiyo ya miaka mingi iliyokuwa ikikikabili kituo cha Afya cha Nagaga.

Msaada huo wa gari la wagonjwa ulitolewa na jana wilayani Masasi na Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Selemani Mzee ambaye alikabidhi gari hilo kwa uongozi wa kituo cha afya cha Nagaga kwa niaba ya Rais Magufuli ikiwa ni utekelezaji wa ahadi yake aliyoitoa mapema mwaka huu wakati akiwa katika ziara ya kikazi wilayani humo ambapo alielezwa kilio cha wakazi wa kata hiyo kupitia mbunge wao wa jimbo la Lulindi, Jerome Bwanausi.

Akizungumza kabla ya makabidhiano, Mzee alisema, Rais Magufuli ametekeleza ahadi yake ya kusaidia kutoa gari la kubebea wagonjwa katika kituo cha afya cha Nagaga na kuagiza wananchi hao wanapaswa kulitumia vema gari hilo ili liweze kutoa huduma iliyokusudiwa kwa muda mrefu.

Mzee alisema Rais Magufuli mapema mwaka huu akiwa katika ziara ya kikazi wilaya Masasi alipokea malalamiko ya wananchi wa kata hiyo kuwa kituo chao cha afya cha Nagaga hakuna gari la kubebea wagonjwa kwa miaka mingi hivyo ahadi hiyo ameamua kuitekeleza kwa vitendo.

Alisema ujio wa gari hilo katika kituo hicho cha afya cha Nagaga ni wazi kuwa sasa tatizo la wananchi hao kubeba wagonjwa kwenye matenga, baiskeli na pikipiki itakuwa ni historia baada ya Rais Magufuli kutimiza ahadi hiyo ya kusaidia hilo.

Fatuma Saidi, mkazi wa kijiji cha Nagaga, alisema kwa niaba ya wananchi wa kata ya Nagaga wanampongeza Rais Magufuli kwa kuwapatia gari hilo la wagonjwa na kwamba awali walikuwa wakitapata adha kubwa ya kubeba wagonjwa na kuwapeleka kupata huduma katika hospitali ya wilaya.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Changwa Mkwazu, aliipongeza serikali kwa kutoa msaada huo wa gari ambalo ni mkombozi mkubwa kwa wananchi wa kata ya Naganga na kituo chao cha afya cha Nagaga.

## HABARI KIMATAIFA

# Obama amkosoa tena Trump corona

**NEWYORK,** Marekani

ALIYEKUWA Rais wa Marekani, Barrack Obama, kwa mara nyingine tena amemkosoa mrithi wake Donald Trump kwa jinsi anavyolishughulikia suala la virusi vya corona.

Katika hotuba kwa hafla iliyopeperushwa kupitia mtandao, alisema kwamba mlipuko wa virusi vya corona umedhihirisha kwamba maofisa wengine hawafanyi kazi walioajiriwa kusimamia.

Amesema kwamba ni 'janga la machafuko' jinsi Trump anavyoangazia suala hilo , katika mkutano uliovuja wiki iliopita.

Rais huyo wa zamani pia aliwahutubia wanafunzi wa shule ya upili katika sherehe iliyoandaliwa na LeBron James na ilikuwa mojawapo ya programu maalum ambayo ilishirikisha watu maarufu kama vile ndugu wa Jonas, Megan Rapinoe, Pharrell Williams na mwanaharakati wa elimu Malala Yousafzai.

**Ugonjwa kama huu unafichua ukosefu wa usawa uliopo na mzigo wa ziada ambao jamii ya watu weusi wamekuwa wakikabiliana nao katika historia ya taifa hili.**

Katika hotuba yake kwa zaidi ya taasisi 10 za wanafunzi weusi na vyuo vikuu, Obama alisema kwamba Covid-19 ilifichua mianya na makosa katika uongozi wa taifa hilo.

"Zaidi ya chochote kile janga hili linaonesha wazi kwamba wengi wa maofisa walio uongozini hawajui wanachofanya," alisema Obama.

Zaidi ya watu 1,200 wamefariki kutokana na virusi vya corona nchini Marekani katika kipindi cha saa 24, kulingana na takwimu mpya kutoka Chuo kikuu cha John Hopkins huku Idadi ya watu waliofariki ni 89,000, ambayo ndio ya juu zaidi duniani.

Obama pia alizungumzia kwa urefu jinsi virusi hivyo vinavyozidi kuiathiri jamii ya watu weusi nchini humo.

"Ugonjwa kama huu unafichua ukosefu wa usawa uliopo na mzigo wa ziada ambao jamii ya watu weusi wamekuwa wakikabiliana nao katika historia ya taifa hili", alisema Obama

Idadi kubwa ya Wamarekani weusi wamekufa na wengine kulazwa hospitalini nchini Marekani kutokana na Covid-19.Rais huyo wa zamani pia alizungumzia kuhusu mauaji ya Ahmaud Arbery aliyekuwa akifanya mazoezi ya kukimbia ambaye alipigwa risasi na maofisa wa polisi weupe mwezi February - katika hotuba yake.

Alisema kwamba ubaguzi wa rangi ulibainika wazi nchini humo wakati mtu mweusi anapofanya mazoezi ya kukimbia na watu fulani wanahisi kwamba wanaweza kumsimamisha na kumuuliza maswali na kumpiga risasi, anapokataa kuwajibu.

Obama amenyamaza kwa kipindi kirefu tangu alipoondoka madarakani mnamo Januari, 2017 na hajawahi kuzungumzia kuhusu vitendo vya mrithi wake, lakini wawili hao wamekabiliana vilivyo katika siku za hivi karibuni, hatua iliomfanya Rais Trump kumshutumu Obama na washauri wake kwa kuendeleza juhudi za kihalifu kuhujumu utawala wale.

"Ni uhalifu mkuu wa kisiasa katika historia ya Marekani , kwa kiwango kikubwa", Rais Trump aliandika katika mtandao wake wa twitter wiki iliopita. **BBC**

# Msimamizi wa ikulu atimuliwa

**NEWYORK,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amemfukuza kazi mkaguzi mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje, Steve Linick.

Kufukuzwa kazi kwa Steve Linick ni hatua ya karibuni ya Rais kumfukuza kazi msimamizi wa serikali.Hadi sasa Trump amewafukuza kazi wasimamizi watatu baada ya kutokutwa na hatia na Baraza la Seneti katika kesi aliyofunguliwa na Baraza la Wawakilishi ya kutumia madaraka vibaya na amekuwa akiwakosoa wengine.

Rais alisema katika barua aliyomtumia Spika wa Baraza la Wawakilishi, Nancy Pelosi, Ijumaa usiku kuwa, hana tena imani na Linick.

"Kitendo cha Rais cha usiku sana wikiendi kumfukuza kazi Mkaguzi Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje kimeongeza kasi mwenendo wake hatari wa kulipiza kisasi dhidi ya wafanyakazi wa umma ambao wana uzalendo waliopewa majukumu ya kusimamia taasisi hizi kwa niaba ya wananchi wa Marekani," Pelosi amesema katika tamko lake Ijumaa.

"Mkaguzi Mkuu Linick ameadhibiwa kwa kuenzi kutekeleza jukumu lake kuilinda Katiba na usalama wa taifa letu, kama anavyotakiwa kufanya hivyo na sheria ya nchi hii na kiapo chake.

Mwakilishi Elliot Engel, mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje ya Baraza la Wawakilishi katika tamko lake amesema ofisi yake ilikuwa tayari imepata taarifa kuwa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu ya Wizara ya Mambo ya Nje ilikuwa imefungua uchunguzi juu ya Waziri wa Mambo Nje, Mike Pompeo.

Kufukuzwa kazi kwa Linick katikati ya uchunguzi huu kunaonyesha wazi kuwa kitendo hiki cha ulipizaji kisasi ni kinyume cha sheria," Engel alisema katika tamko lake.Linick aliteuliwa kuwa Mkaguzi Mkuu na Rais Barack Obama. Kushiriki kwa Linick katika mchakato wa kesi ya kumuondoa madarakani rais uliishia katika kutoa muhtasari kwa kamati mbalimbali za bunge na kuwapatia wabunge nyaraka kutoka kwa mwanasheria wa rais, Rudy Giulian.



Mji wa Wuhan nchini China ambapo mlipuko wa virusi vya ugonjwa wa corona ulianzia, juzi yalifanywa majaribio 222,675, kwa mujibu wa mamlaka ya afya ya nchini humo jana. **PICHA: REUTERS**

# Mshukiwa mauaji ya kimbari mbaroni

**KIGALI,** Rwanda

FÉLICIEN Kabuga, mmoja wa washukiwa wakuu wa mauaji ya kimbari ya Rwanda, amekamatwa karibu na mji wa Paris, Wizara ya Sheria ya Ufaransa imetangaza.

Kabuga ameshikiliwa na polisi mjini Asnières-Sur-Seine, eneo ambalo alikuwa anaishi kwa kutumia majina bandia. Marekani ilitoa dau la dola milioni 5 kwa atakayeweza kutoa taarifa kuhusu bwana Kabuga ili aweze kukamatwa.

Mahakama ya kimataifa ya mauji ya kimbari yaliyotokea Rwanda Kabuga mwenye umri wa miaka 84 kwa uhalifu dhidi ya ubinadamu anadaiwa kuwa mfadhili mkuu wa Wahutu ambao waliuwa watu 800,000 mwaka 1994.Walikuwa wanawalenga kundi dogo la jamii ya Tutsi pamoja na wapinzani wao siasa.

Kabuga alizaliwa katika eneo la kaskazini mwa Rwanda ambako alijilimbikizia mali kutokana na biashara ya majani ya chai miaka ya 1970 na kuwekeza katika biashara tofauti nchini humo, mataifa jirani na ng'ambo.

Alikuwa mwandani wa karibu wa chama tawala cha MRND na baba mkwe wa rais Juvénal Habyarimana.Kabuga anayetuhumiwa kuwa mfadhili mkuu wa mipango ya kutekeleza mauaji ya kimbari , alikuwa mwenye hisa mkuu katika kituo cha radio ya kibinafsi RTLM ambacho kililaumiwa kwa kuwahamasisha watu wa jamii ya Kihutu kuwaua wenzao wa Watutsi.

Kutokana na utajiri wake, baada ya mauaji ya kimbari, Kabuga, alifanikiwa kujificha katika mataifa mengi hadi alipokamatwa Mei 16,2020.

Félicien Kabuga ni mfanyabiashara maarufu nchini Rwanda, ambaye alichukuliwa kuwa mtu tajiri zaidi nchini humo kabla ya kufanyika kwa mauaji ya kimbari ya mwaka 1994.

"Kila mmoja amefurahia hatua ya kukamatwa kwake, kila mmoja amekuwa akisubiri habari hizi kwa sababu alikuwa katika orodha ya washukiwa wa mauaji ya kimbari" Vlerie Mukabayire kiongozi wa chama cha wajane wa mauaji ya kimbari AVEGA aliiambia BBC.

"Ni jambo la kutia moyo sana kwamba hatimaye atafikishwa mbele ya haki kuwajibikia kile alichokifanya" aliongeza.

Ahishakiye Naphtal, Katibu mkuu wa Ibuka, chama Tanzu cha wahathiriwa wa mauaji ya kimbari anasema hizi ni habari njema kwa waliopona mauaji hayo, kusikia Kabuga amekamatwa baada ya miaka 26.

Ahishakiye anasema Ufaransa chini ya uongozi wa Rais Emmanuel Macron imebadili mtazamo wake kuhusu watuhumiwa waliotoka katika mauaji ya kimbari ya Rwanda, 'Hali ambayo imechangia hatua ya kumkamata' anasema.

Mahakama ya Umoja wa mataifa inayoshughulikia kesi ya mauaji ya kimbari ya Rwanda, imesema ilikuwa imetoa waranti ya kumkamata na kutangaza kukamata.

Mahakama hiyo ina vitengo mjini Arusha, Tanzania na The Hague, Uholanzi. Kitengo cha mshitaka nchini Rwanda kimepongeza kukamatwa kwa Kabuga katika Twitter yake, ikisema kuwa Rwanda itaendelea kushirikiana na mahakama maalum ya Umoja wa Mataifa kuhakikisha haki inatolewa.

Mwendeshaji mkuu wa mashitaka wa kitengo cha mahakama ya Umoja wa Mataifa kwa ajili ya Rwanda-'International Residual Mechanism for Criminal Tribunals' (IRMCT) mjini Hague - mahakama inayosikiliza kesi za uhalifu wa vita za Rwanda na iliyokuwa Yugoslavia - alisema polisi wa Ufaransa walimkamata bwana Kabuga siku ya Jumamosi, baada ya matokeo ya operesheni ya pamoja ya uchunguzi wa muda. **BBC**




# HAALAND: SIKUSHANGAA KUFUNGA BUNDESLINA

**DORTMUND,** Ujerumani

ERLING Haaland kwa kujiamini amedai halikuwa jambo la kushangaza kwake kurudi dimbani na kufunga, wakati akiisaidia Borussia Dortmund kupata ushindi mkubwa dhidi ya Schalke kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, juzi.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Norway mwenye umri wa miaka 19, alifunga bao la ufunguzi katika ushindi wa 4-0 pale kwenye dimba la Signal Iduna Park Jumamosi, wakati Ligi ya Ujerumani iliporudi kuendelea baada ya kusimama kwa miezi miwili kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Raphael Guerreiro aliongeza mawili kwa kikosi hivyo, huku Thorgan Hazard akifunga la mwisho wakati Dortmund wakipata ushindi huo mtamu.

Haaland ambaye bao lake hilo lilikuwa la 10 katika mechi tisa za Bundesliga alikubali kwamba, bado hakuwa kwenye kasi yake.

"Bila shaka, siko sawa. Sijacheza mechi kwa wiki saba, sikuwa fiti sana," alisema akiiambia tuvoti ya Bundesliga.

"Lakini najua sijajifua sana kipindi hiki, na sikushangaa kufunga, hapana."

Dortmund baada ya ushindi huo wamewakaribia vinara wa ligi hiyo, Bayern Munich wakipishana pointi moja, ambapo Bavaria wao walikuwa wanacheza jana Jumapili.

# Madrid na ofa kwa Mo Salah – Kocha

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid ilituma ofa kwa nyota wa Liverpool, Mohamed Salah, mwezi ambao aliwaongoza kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2018, kwa mujibu wa mmoja wa afisa wa benchi la ufundi la timu ya Taifa ya Misri.

Salah alifurahia msimu bora wa 2017-18, akifunga mabao 32 kwenye Ligi Kuu ya England na kutoa pasi za mwisho 10.

Hata hivyo, alimaliza msimu huo kwa machungu baada ya kuumia bega wakati alipogongana na Sergio Ramos katika dakika za mwanzo za fainali ya Ligi ya Mabingwa mjini Kiev, Ukraine.

Vijana hao wa Jurgen Klopp walipoteza fainali hiyo kwa kichapo cha mabao 3-1 na Salah aliweza kuwa fiti kwa wakati na kujiunga na kikosi cha Misri kwenye michuano ya Kombe la Dunia nchini Urusi.

Nyota huyo wa zamani wa AS Roma, alifunga mabao mawili kwa 'Farao' hao na walipoteza mechi zote na kutolewa hatua ya makundi.

Kwa mujibu wa mchezaji wa zamani wa Misri, Hany Ramzy, Salah alijadiliana kuhusu kutakiwa na Madrid na kocha wa timu ya taifa, Hector Cuper, wakati wakiwa mwenye kambi ya mazoezi nchini Uswisi.

Ramzy ameiambia televisheni moja ya nchini Misri, OnTimes Sports kwamba, alikuwapo kwenye majadiliana hayo.

"Nilizungumza na Salah na aliniambia Real Madrid wamemtumia ofa ya kumtaka," alisema.

"Ofa ilikuwa nzuri sana, lakini Salah alijadiliana na mimi na Cuper, na aliamua kubakia Liverpool kwa sababu alikuwa anafurahia maisha pale."






# Man City waitega Bayern kwa Sane

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City, imeweka masharti ya kumuachia mshambuliaji wao, Leroy Sane, anayeripotiwa kuwa kwenye mipango mizuri ya kujiunga na Bayern Munich ya Ujerumani.

Man City wameitaka klabu hiyo kumtoa beki wao wa kushoto, David Alaba, ili awe sehemu ya uhamisho wa Sane.

Mkataba wa Sane na Man City utafikia tamati mwaka 2021, na nyota huyo bado hajaanza mazungumzo na klabu hiyo kwa ajili ya kusaini mkataba mpya, huku taarifa zikieleza mshambuliaji huyo anatamani kuondoka hapo jijini Manchester.

Wachezaji wengi raia wa Ujerumani, wanaamini kucheza Bayern Munich, ndio njia rahisi ya kupata nafasi kwenye timu ya taifa.

Kwa mujibu wa gazeti la Bild, mkataba wa Alaba utafikia tamati mwaka 2021 na uongozi wa Bayern upo tayari kumuuza kama atataka kuondoka kuanzia mwishoni mwa msimu huu.

Taarifa zingine zinaeleza kuwa Man City, walikuwa wanahitaji kumsajili beki wa kushoto kati ya Lucas Digne na Ben Chilwell, hivyo dili hilo huenda likafa kama watafanikiwa kumsajili Alaba.

Alaba ni moja ya mabeki bora wa pembeni, wenye uwezo wa kucheza nafasi zaidi ya mbili uwanjani.

## HABARI MICHEZO

# Emery asimulia ugomvi wake na Ozil Arsenal

**LONDON,** England

UNAI Emery amefunguka na kueleza uhusiano wake ulivyokuwa na Mesut Ozil pale Arsenal na kusema kiungo huyo "anatakiwa kujichunguza mwenyewe, kwa tabia yake na majukumu yake."

'Washikabunduki' hao walimteua Emery kama mrithi wa Arsene Wenger Mei mwaka 2018, lakini miezi 18 baadaye alifukuzwa huku Arsenal ikianza vibaya msimu wa 2019-20.

Uhusiano ya Emery na Ozil mara kwa mara yalipamba vyombo vya habari na Mjerumani na mshindi huyo wa Kombe la Dunia akajikuta nje ya kikosi chini ya kocha huyo raia wa Hispania.

Ozil alipewa mkataba mpya pale Arsenal Januari mwaka 2018, ikiwa ni miezi minne tu tangu kuteuliwa kwa Emery, na nyota huyo wa zamani wa Real Madrid alionekana ni mchezaji ambaye hajitumi kwa kocha wake huyo.

"Mwishoni anatakiwa kujiangalia yeye mwenyewe. Kuhusu tabia yake na majukumu yake," alisema Emery alinukuliwa na gazeti la Daily Mail.

"Nilijaribu kumsaidia kwa namna fulani Ozil. Kwa kipindi changu chote cha ukocha, wachezaji wenye vipaji huwa navutiwa nao na wamekuwa wanacheza kwa ubora wao au wanapoteza kiwango chao wakiwa nao au wanapoteza kiwango chao wakiwa na mimi.

"Mara zote nilikuwa na mtazamo chanya sana kwake yeye na kwa kila kitu ambacho alikuwa anahusika nacho, lakini tabia yake na kutokujituma kwake uwanjani kukafanya mambo kuwa tofauti kabisa.

"Ozil alikuwa na uwezekano wa kuwa mmoja wa nahodha wetu, lakini kwenye vyumba vya kubadilishia nguo alikataa kuwa nahodha.

Emery pia akakumbushia machungu aliyoyapata kwenye mchezo wa fainali ya Ligi ya Europa wakati walipochapwa 4-1 na Chelsea, namna Ozil alivyokataa kuzungumza naye.





# GUARDIOLA KOCHA BORA WA WAKATI WOTE – SILVA

**MANCHESTER,** England

BERNARDO Silva amemsifia Pep Guardiola, akimtaja bosi huyo wa Manchester City kuwa "mmoja wa makocha bora zaidi kuwahi kutokea."

Guardiola ameiongoza City kutwaa mataji mawili ya Ligi Kuu, matatu ya EFL moja na FA na mawili ya Ngao ya Jamii tangu alipotua hapo mwaka 2016.

Raia huyo wa Hispania, ambaye pia alifurahia mafanikio kule Barcelona na Bayern Munich, anatajwa kama mmoja wa makocha bora wa wakati wote duniani.

Silva amepaza sauti kumsifia kocha huyo mwenye umri wa miaka 49 kwa mchango wakati akiwa katika klabu hiyo ya Ligi Kuu, akisema: "Binafsi, nimejifunza mengi si tu kutoka kwake, lakini pia kwa wachezaji wenzangu, tangu nilipowasili Manchester City.

"Yeye pia ni mmoja wa makocha bora kuwahi kutokea. Ni jambo jema kuwa na sisi."

Silva pia amesifia uwezo wa Guardiola kuibadilisha City kwa stali ya uchezaji, huku timu hiyo ikipata pointi 100 wakati wakishinda taji la Ligi Kuu ya England msimu wa 2017-18 kwa kuvunja rekodi.

"Najua wachezaji wenzangu, ushawishi alionao tangu alipowasili Manchester City umekuwa mkubwa sana," amesema mchezaji huyo raia wa Ureno.

"Unaweza kuona kutokana na matokeo yake, kwa mataji aliyobeba kwa kipindi cha misimu mitatu iliyopita. Tangu nimekuja hapa nimeshinda mataji kadhaa."

# *Klabu Serie A kuanza mazoezi ya pamoja*

**ROME,** Italia

TIMU za Ligi Kuu ya Italia, Serie A, zimeruhusiwa kuanza mazoezi ya pamoja leo Jumatatu, Waziri Mkuu wa Italia, Giuseppe Conte (pichani) ametangaza.

Klabu zilipewa ruhusa ya kuanza mazoezi Mei 4, ingawa ilikuwa ni kwa mchezaji mmoja mmoja.

Ikiwa sehemu ya kulegeza masharti ya 'lockdown', Conte ameruhusu timu kuanza mazoezi leo Jumatatu kwa ajili ya maandalizi ya kurejea kwa Ligi Kuu.

"Timu zitaanza mazoezi Mei 18 (leo Jumatatu), kwa pamoja," alisema wakati wa hotuba yake ya Jumamosi.

Uamuzi huo unaifanya Ligi Kuu ya Serie A kukaribia kurudi, ingawa Conte alisema yeye na Waziri wa Michezo, Vincenzo Spadafora, bado watafuatilia mbinu za kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona na ikiwezekana wataiga hatua zilizochukuliwa na Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, iliyorudi tena mwishoni mwa wiki.

Serie A na Shirikisho la Soka la Italia, (FIGC) bado hawajafikia makubaliano ya sheria za kimatibabu zilizowekwa na serikali wakati ligi hiyo itakaporejea.

Idara ya afya ya nchini humo inataka klabu yoyote kuwekwa karantini kwa siku 14 kama mchezaji wake mmoja anakutwa na maambukizo ya virusi vya corona, hali ambayo wanaiona itakuwa ngumu kwao.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LAMPARD: GIROUD, WILLIAN HAWAUZWI

●●● Arsenal, Tottenham na Liverpool sasa kugonga mwamba mbio saini ya...

**LONDON,** England

KOCHA wa Klabu ya Chelsea, Frank Lampard, huenda akabadili mpango wa kuwaachia wachezaji wake wawili, Willian na Olivier Giroud, ambao mwishoni mwa msimu huu watakuwa wachezaji huru baada ya mikataba yao kumalizika.

**Mikataba ya wawili hao inatarajiwa kufikia kikomo Juni 30, mwaka huu lakini Lampard amesema anahitaji kuendelea kuwa na uimara wa kikosi chake na hafikirii kumuachia mchezaji yeyote.**

Lampard anafikiria kuanza mazungumzo na wachezaji hao wawili ambao tayari wameshaanza kutajwa kwenye mipango ya usajili ya baadhi ya klabu za ndani na nje ya England.

"Tuna wachezai wenye hadhi kubwa ya kupambana, sitegemei kuona yeyote anaondoka kwenye kikosi changu, nahitaji kuwa nao wote kwa msimu ujao," alisema Lampard alipohojiwa na Sky Sports.

"Wachezaji ambao mikataba yao ipo ukingoni, klabu itaanza utaratibu wa kufanya nao mazungumzo, na nina matumaini mambo yatakua mazuri.

"Kila mmoja anatamani kuiona Chelsea ikiendelea kuwa na kikosi kama ilivyo msimu huu, nina matarajio makubwa na kila mchezaji aliye kikosini kwa sasa na kila mmoja ana nafasi yake pale ninapomuhitaji kwa michezo husika."

Tayari Willian alianza kuhusishwa na mipango ya kuwania na klabu za jijini London Arsenal na Tottenham Hotspur, pia klabu ya Liverpool nayo ilitajwa kwenye mpango huo.

Giroud alikuwa akitajwa zaidi kuwaniwa na miamba wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Inter Milan, huku pia vigogo wa Ligi Kuu ya Ufaransa PSG wakionekana kumnyatia Mfaransa huyo.

## ZISIKUPITE

### MBAPPE AFUNGUKIWA PSG

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe, hatalazimisha kuondoka Paris St-Germain kipindi kinachokuja cha majira ya joto, kwa sababu ya athari za kifedha kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, ataendelea kubakia kwa mabingwa hao wa Ligue 1 kwa msimu mmoja zaidi. ***(L'Equipe)***

### XAVI HOFU KWA MANE

KIUNGO wa zamani wa Barcelona na Hispania, Xavi ana shaka kama mshambuliaji wa Liverpool na Senegal, Sadio Mane mwenye umri wa miaka 28, na mshambuliaji wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang, 30, ambaye anaichezea Arsenal, kama wataweza kufiti kwenye soka la pale Nou Camp. ***(Metro)***

### JUVE YAKARIBIA KWA POGBA

KLABU ya Juventus inakaribia kumsajili kiungo wa Ufaransa, Paul Pogba, mwenye umri wa miaka 27, kutoka Manchester United na watajaribu kumtumia Mfaransa mwenzake, Adrien Rabiot, 25, kama sehemu ya usajili huo. ***(L'Equipe)***

### 'KANTE, JORGINHO HAWAUZWI'

CHELSEA wako tayari kuwauza baadhi ya wachezaji wake katika kikosi cha kwanza ili kupata fedha za kujiimarisha msimu huu, lakini hawana nia ya kupokea ofa ya kuwauza wachezaji N'Golo Kante mwenye umri wa miaka 29 na Jorginho, 28. ***(ESPN)***

### MESSI AMSIFIA MARTINEZ

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Lionel Messi, amesifia ubora wa mshambuliaji wa Inter Milan na raia mwenzake wa Argentina, Lautaro Martinez mwenye umri wa miaka 22, ambaye ametajwa kuwaniwa na klabu za Hispania. ***(Sport, via Metro)***

### CHELSEA KUMUUZA MORATA

KLABU ya Chelsea inapanga kupokea pauni milioni 48.5 kutoka kwa Atletico Madrid kwa ajili ya mshambuliaji wake, Alvaro Morata raia wa Hispania mwenye umri wa miaka 27, kipindi cha majira ya joto na watatumia fedha hizo kumsajili Sancho. ***(Sun on Sunday)***

### ZIDANE BADO NA POGBA

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, bado ana matumaini makubwa ya kumshawishi Paul Pogba mwenye umri wa miaka 27, kutua hapo Santiago Barnabeu kutoka Manchester United kipindi kinachokuja cha majira ya joto. ***(Mundo Deportivo)***

### MNIGERIA RUKSA ARSENAL

KOCHA wa Klabu ya Club Bruges, Philippe Clement, amesema anatarajia mshambuliaji wa Nigeria Emmanuel Dennis mwenye umri wa miaka 22, ambaye amekuwa akihusishwa na Arsenal, Newcastle United na Wolves, kuondoka klabuni hapo. ***(La Derniere Heure, via Birmingham Mail)***

### BARCA, REAL KWA SANCHO

BARCELONA na Real Madrid zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili winga wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho, lakini Manchester United ndio inayoonekana kuwa kwenye nafasi nzuri kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 20. ***(Athletic, via Star on Sunday)***

HABARI MICHEZO

## Serikali ya Z'bar yapika waamuzi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limeshauriwa kutoa kipaumbele katika mpango wa kufundisha waamuzi vijana walio chini ya umri wa miaka 17 ili kukabiliana na changamoto ya uhaba wa marefa hapa nchini.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkufunzi wa Waamuzi, mwamuzi mstaahafu wa Fifa, Ramadhani Ibada Kibo, alisema mpango huo utaweza kutanua wigo wa kuwapata waamuzi ambao watadumu kwa muda mrefu katika fani hiyo kutokana na umri wao kuwa mdogo.

Alisema mpango huo wa kusomesha waamuzi hao vijana ili kuingia katika fani hiyo utalisaidia shirikisho hilo kuwapata waamuzi wanaoendana na kasi ya soka la sasa kutokana na mipango mingi ya soka kulenga vijana.

Aidha, alisema kwa sasa mpango huo kwa Zanzibar umepiga hatua kwa kushirikiana na wizara ya elimu pamoja na wizara ya michezo kwa kuwa na akademi ambayo inasimamia kwa kuwapa mafunzo waamuzi hao.

"Tunaishukuru serikali kwa hapa tulipofikia maana wao ndio wanawahudumia kila kitu waamuzi ambao tupo nao katika akademi iliyopo huko Kama, na pia wanasimamia masuala yote ya masomo yao, hili ni jambo zuri na linatia moyo na hii itasaidia kuwapata marefa wenye uwadilifu na kazi zao." alisema.

Jumla ya waamuzi 21 chini ya umri wa miaka 17, wapo katika kituo hicho cha mafunzo ya waamuzi ambacho kinasimamiwa na serikali kupitia wizara ya elimu na na ile ya michezo lengo kubwa likiwa ni kuitanua fani hiyo na kuondokana na uhaba wa waamuzi vijana.

## Adam sasa fiti kukimbiza JKT

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kukaa chumba cha majeruhi kwa mwezi mzima akiuguza jeraha la goti, mshambuliaji wa JKT Tanzania, Adam Adam, amesema kwa sasa anaendelea vizuri na yupo fiti kurejea dimani pindi ligi hiyo itakapoendelea tena.

Akizungumza na Nipashe jana, Adam alisema kwa sasa anashukuru hali yake imeimarika na tofauti na mwanzo.

"Nashukuru, naendelea vizuri na ninafanya mazoezi ili kuuweka sawa mwili wangu kujiandaa na ligi," alisema Adam ambaye hadi anapata majeraha hayo, alishatupia mabao sita kwenye Ligi Kuu.

Aidha, aliwashukuru wachezaji wenzake pamoja na uongozi kutokana na ushirikiano waliompa siku zote akiwa anauguza majeraha hayo.

"Naushukuru uongozi wangu walinisaidia na kunijali kipindi chote ambacho nilikuwa mgonjwa mpaka sasa," alisema.

# AZAM WAZIACHIA SIMBA, YANGA STRAIKA WA KOTOKO



**Na Saada Akida**

LICHA ya kuhusishwa kuwa kwenye mbio moja na Simba na Yanga kuwania saini ya mshambuliaji wa Klabu ya Asante Kotoko ya Ghana, Sogne Yacouba (pichani), Azam FC imejiweka kando baada ya kusema "hapana si huyo".

**Kwa muda mrefu Simba, Yanga na Azam zimekuwa zikielezwa kuwa kwenye mbio moja ya kusaka huduma ya straika huyo raia wa raia wa Burkina Faso.**

Lakini akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Mtendaji Mkuu Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema hawapo katika mbio za kumgombea mchezaji huyo ingawa mipango yao ni kusajili mshambuliaji mmoja kutoka nje ila huyo anayetajwa kuhusishwa na klabu kongwe hapa nchini hayupo kwenye rada zao.

Alisema kwa misimu mitatu safu yao ya ushambuliaji haikufikia kiwango kama ilivyokuwa awali kabla ya kuondoka baadhi ya washambuliaji wao wawili Kipre Tchetche na John Bocco.

"Tutasajili mshambuliaji mmoja kutoka nje na mipango imeanza, ila si kweli kwamba tunazungumza au kumhitaji nyota huyo wa Kotoko," alisema Popat.

Alisema kwa kipindi kirefu wameona tatizo la safu yao ya ushambuliaji kwa kutokuwa tishio kama ilivyokuwa enzi za Tchetche na Bocco, hivyo wamepanga kuimarisha kuelekea msimu mpya.

"Tumeangalia kikosi chetu, ushambuliaji ndio tatizo kubwa, hivyo mipango yetu kwa sasa ni kusajili mshambuliaji mmoja hatari wa kimataifa ambaye atakuja kuongeza nguvu kwa watakaobakia hapa," alisema Popat.

KAZI MOJA TU...



Nahodha wa Yanga, Papy Tshishimbi (kushoto) akifanya mazoezi na rafiki zake mchangani, kipindi hiki klabu yake ikiwa imesitisha mazoezi ya pamoja kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona (COVID-19). **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Kikoti agomea vigogo Ligi Kuu Bara*

**Na Shufaa Lyimo**

KIUNGO mshambuliaji wa Namungo FC yenye maskani yake Ruangwa mkoani Lindi, Lucas Kikoti, amesema "niacheni kwanza" kwa sababu mkataba wake unamfunga kuzungumza na klabu yoyote kwa sasa.

Kikoti amekuwa akihusishwa na klabu nyingi za Ligi Kuu ikiwamo Yanga, kuelekea dirisha la usajili lijalo. Akizungumza na Nipashe jana, kiungo huyo alikiri kufuatwa na viongozi wa timu kubwa hapa nchini wakiwa na lengo la kuhitaji huduma yake kuelekea dirisha la usajili lijalo, lakini akazitaka kuketi meza moja ya mazungumzo na Namungo FC.

"Kuna viongozi wa klabu kubwa hapa nchini wananitaka kwa ajili ya msimu ujao, lakini nimegoma kuzungumza nao kwa kuwa mkataba wangu bado haujamalizika," alisema Kikoti ambaye ameifungia Namungo mabao manne msimu huu.

Hata hivyo, Kikoti alizitaka timu zinazohitaji huduma yake msimu ujao kufuata taratibu zote zinazotakiwa ikiwa ni pamoja na kukaa meza moja na viongozi wa klabu yake.

"Wafuate taratibu zote za usajili ili kuepusha matatizo hasa ukizingatia dirisha hilo mpaka sasa bado halijafunguliwa rasmi," alisema.

Alisema klabu za hapa nchini zimekuwa zikihitaji huduma ya wachezaji wa Namungo baada tu ya kuonekana kujituma kwa bidii kabla Ligi Kuu Bara kusimamishwa Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona.

Winga huyo alisema ushirikiano pamoja na nidhamu ndio zimewapa mafanikio Namungo kwa kumsikiliza kwa makini kocha wao mkuu, Mnyarwanda Hitimana Thierry.

Aliongeza kuwa kwa sasa anaendelea na mazoezi binafsi na kudai endapo Ligi Kuu itarejea ataendeleza ushindani ili kuifikisha mbali Namungo, huku akiwataka mashabiki wao kuendeleza ushirikiano.

# Michezo

Jumatatu Mei 18, 2020

Nipashe





Lampard: Giroud, Willian hawauzwi

UKURASA 22

LIGI YAJA...



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, akizungumza na waumini wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Chato mkoani Geita jana, ambapo alieleza endapo hali ya maambukizo ya virusi vya corona itaendelea kupungua kama ilivyo kwa sasa, wiki hii ataruhusu ligi kuendelea. **PICHA: IKULU**

## Yanga yaanika nafasi 4 kusajili

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Yanga umeweka wazi idadi ya wachezaji sita ambao kwa sasa wanawindwa kwa ajili ya kuongeza nguvu katika kikosi cha msimu ujao.

Tayari ulishaeleza kuwa Kocha Mkuu, Mbelgiji Luc Eymael (pichani) ameacha ripoti ambayo inahitaji kufanyiwa kazi kuelekea usajili wa dirisha kubwa, lakini jana uongozi umeainisha rasmi nafasi ambazo wametakiwa kusajili.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema katika mapendekezo hayo ya Eymael ametaka kufanyika usajili wa washambuliaji wawili, kiungo mkabaji na beki mmoja wa kimataifa.



Alisema katika mapendekezo hayo hajaweka wazi majina ya wachezaji ambao amewataka lakini ameuomba uongozi kushirikiana naye katika mchakato huo wa usajili kuletewa mchezaji ambaye atakuwa ameridhika naye.

"Msimu ujao Yanga itasajili wachezaji sita wapya, dirisha la usajili halijafunguliwa kwa hiyo ni ngumu kuweka bayana ni nani na nani wanasajiliwa, kitu kikubwa tusubiri kuona dirisha likifunguliwa.

"Tumepanga kuboresha kikosi chetu ikiwamo kuongeza nguvu, ila sasa hivi tunasubiri ligi kumalizika kama inarejea kwani tuna malengo ya kufanya vizuri mechi tulizokuwa nazo mkononi pia Kombe la FA," alisema Bumbuli.

# JPM atoa tamko ligi kurejea

**Na Mwandishi Wetu**

### ●●● Asema hali ya corona ikiendelea hivi, wiki hii ataruhusu irejee kwa kuwa...

KWA mara nyingine tena Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, amewaweka wadau wa soka mguu sawa baada ya kueleza kufurahishwa na idadi ya wagonjwa wa virusi vya corona katika vituo vilivyotengwa nchini kupungua sana, hivyo anaangalia wiki hii kama hali itaendelea kama ilivyo, ataamua kuruhusu michezo iendelee.

**Rais Magufuli alitoa kauli hiyo jana wakati alipoungana na waumini wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Chato mkoani Geita kusali ibada ya Jumapili iliyoongozwa na Mchungaji Thomas Kangeizi.**

Kauli hiyo ya Magufuli ilikuja baada ya kutoa takwimu za mpaka jana Mei 17, kuwa Hospitali ya Amana (Dar es Salaam) iliyokuwa na wagonjwa 198 imebakiwa na mgonjwa 12, Mloganzila iliyokuwa na wagonjwa 30 imebakiwa na sita, Kituo cha Lulanzi (Kibaha) kilichokuwa na wagonjwa zaidi ya 50 lakini sasa kimebakiwa na 22, Agha Khan kikibakiwa na wagonjwa 31 huku Hindu Mandal kikibakiwa na wagonjwa 16 tu.

Aliendelea kueleza kuwa Hospitali ya Regency wamebaki wagonjwa 17, TMJ saba, Rabinisia 14, Moshono (Arusha) 11, Buswelu na Misungwi kila moja wagonjwa wawili, huku Longido, Karatu, Ukerewe, Magu, Mkuyuni, Nyahunge, Sengerema, Kongwa, Kondoa na Kwimba zikiwa hazina mgonjwa hata mmoja, lakini pia Sekou Toure, Dodoma kila moja ikibaki na wagonjwa wawili kutoka zaidi ya 40 wa awali.

"Mimi namwamini Mungu na Mungu amejibu maombi yetu, tumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutusikiliza na tuendelee kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huu wa corona," alisema Magufuli na kuongeza:

"Kwa hali hii ninavyoona kama ikiendelea hivi kwa wiki hii, nimepanga kufungua vyuo ili wananfunzi waendelee kusoma, lakini pia nimepanga kuruhusu michezo iendelee maana ni moja ya burudani kwa Watanzania."

Hiyo ni mara ya pili kwa Rais Magufuli kutoa kauli hiyo ya kuonyesha dhamira ya kuruhusu michezo kurejea nchini baada ya awali Mei 3, akiwa Chato mkoani Geita wakati akimwapisha, Dk. Mwigulu Nchemba kuwa Waziri wa Katiba na Sheria kuchukua nafasi iliyoachwa wazi na Marehemu Balozi Dk. Augustine Mahiga, aliyefariki dunia Mei Mosi, mwaka huu, kusema kuwa kwa siku zinazoendelea anafikiria kuruhusu ligi za mipira ziendelee na anachosubiri ni ushauri kutoka kwa wataalamu wake.

Ligi Kuu Bara ilisimama tangu Machi 17, mwaka huu baada ya serikali kupiga marufuku shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu ikiwamo michezo yote kutokana na mlipuko wa virusi vya corona vinavyoitesa dunia kwa sasa ambavyo hadi kufikia jana jioni jumla ya wa 4,750,322 duniani kote walishapata maambukizo, huku kati yao waliopona wakiwa ni 1,830,489 na waliopoteza maisha 313,797.

Tayari Shirikisho la Soka nchini (TFF), limefanya kikao na Bodi ya Ligi (TPLB), na kutoka na kauli moja ya ligi hiyo kurejea mapema Juni endapo tu serikali itatoa ruksa ya kuendelea kwa shughuli za michezo.

Hadi Liigi Kuu inasimama, Simba ndiyo iliyopo kileleni ikiwa na alama 71 ikifuatiwa na Azam FC pointi 54 baada ya timu zote kushuka dimbani mara 28 na Yanga ina pointi 51 katika nafasi ya tatu zilizotokana na mechi 27.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >